# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MUUNGANO

## MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI WA KIJIJI, KATA YA NANGARU, TARAFA YA NANGARU, WILAYA YA LINDI, MKOA WA LINDI

**IMEFADHILIWA NA:**

**SERIKALI YA NCHI YA NORWAY KUPITIA MRADI WA MKUHUMI KWA AJILI YA JAMII NA MAENDELEO YA MISITU UNAOTEKELEZWA NA TFCG NA MJUMITA**

**NOVEMBER, 2010**

**MUHTASARI WA UTENDAJI**

Kijiji cha Muungano kipo katika Kata ya Nangaru, Tarafa ya Nangaru katika Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi, eneo lake lipo kati ya jira 8904029 na 8918061 Kaskazini na 537910 na 551306 Mashariki Kijiji cha Muungano ni miongoni mwa vijiji 134 vya Wilaya ya Lindi.

Kijiji hiki ni cha asili na kipo umbali wa kilometa 55 kutoka makao makuu ya Wilaya, mwishoni mwa barabara itokayo Mtange kwenda Nangaru. Kipo katika kata ya Nangaru, Tarafa ya Nangaru, Wilaya ya Lindi. Kimepakana na kijiji cha Mkombamosi kwa upande wa Mashariki na kwa upande wa Magharibi kijiji kimepakana na Kiwawa, kwa upande wa kusini kijiji kimepakana na kijiji cha Ruhoma na Milola magharibi na kwa upande wa Kaskazini kijiji kimepakana na Namkongo na Lihimilo. Kijiji kina ukubwa wa hekta 10,479.00

Kijiji cha Muungano kinakabiliwa na matatizo yafuatayo: Ukosefu wa maji safi na salama, Ukosefu wa shule ya msingi, Ukosefu wa umeme, Ukosefu wa Zahanati, Eneo kubwa la utawala, Ukosefu wa soko la kuuzia mazao, Barabara duni, Wanyama waharibifu wa mazao, Ukosefu wa zana bora za kilimo na pembejeo na uchomaji moto holela.

Matatizo haya yanayowakabili wanakijiji wa Muungano yanaweza kuisha iwapo fursa zilizopo ndani ya kijiji na nje ya kijiji zitatumika ipasavyo. Fursa zilizopo kijijini ni pamoja na ardhi ya kutosha na yenye rutuba, Mazao ya biashara, Barabara ya zamani, Wataalam ngazi ya kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Uongozi, (serikali ya kijiji pamoja na Halmashauri ya kijiji), Nguvukazi, Wahisani, Kamati mbalimbali za kijiji, Maliasili na rasilimali za ardhi kama vile uoto, maji, udongo n.k. pamoja na Mradi wa MKUHUMI ambao unahamasisha utunzaji wa Misitu na Mazingira kwa ajili ya Maendeleo ya wanakijiji.

Matumizi bora na endelevu yatasaidia kupunguza matatizo hayo. Sheria zitawezesha utatuzi wa migogoro ya matumizi ya rasilimali za ardhi zilizopo kijijini. Sheria zinazohusika ni kama vile sheria za Ardhi, sheria za maji, sheria za misitu n.k. katika kutatua matatizo yanayo kikabili kijiji na kuwa na matumizi endelevu ya maliasili na rasilimali zilizopo.

Katika kijiji cha Muungano wanakijiji wamependekeza matumizi ya ardhi yafuatayo:- Eneo la kilimo, eneo la vyanzo vya maji, eneo la makazi, eneo la huduma za jamii,eneo la malisho, eneo la msitu wa hifadhi, eneo la Matambiko na eneo la Makaburi

**SHUKRANI**

Mradi wa Mpango wa Kupunguza uzalishaji wa Hewa ya Ukaa inayotokana na ukataji miti hovyo na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) kwa ajili ya jamii na utunzaji wa misitu, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na Timu ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya (PLUM) na wataalam kutoka Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi wanatoa shukrani za dhati kwa mchakato wa kuwawezeha wananchi wa kijiji cha Muungano kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji.

Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji ni mojawapo ya misingi muhimu ya kuwawezesha wanakijiji kuwa na mafanikio ya uhakika katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, mpango huu ni nyenzo muhimu ambayo haina budi kutumika katika kufanikisha malengo ya matumizi na uhifadhi endelevu wa ardhi na rasilimali zake zote katika ngazi ya kijiji. Shukrani za pekee ziwaendee Wataalamu wa Mradi wa MKUHUMI, Timu ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Wilaya ya Lindi pamoja a wataaalam wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ambao wamewezesha shughuli hii kuanza kama ilivyopangwa.

Wanakijiji wa kijiji cha Muungano wameweza kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali ili waweze kutumia ardhi yao na maliasili zilizopo kwa ubora zaidi na uendelevu. Matarajio ni kwamba matatizo yanayowakabili wanakijijiji wa Muungano hivi sasa yanayohusiana na matumizi ya ardhi na maliasili zilizopo juu na chini yake, ikiwa ni pamoja na usalama wa miliki zao za ardhi, yatapungua au kuisha kabisa kutokana na utekelezaji wa mpango wao huu wa matumizi ya ardhi ya kijiji waliojiwekea. Na wataweza kuuhuisha mara kwa mara kadri haja na mahitaji yatakavyojitokeza.

Wawezeshaji waliofanikisha kuanzisha mchakato huu ni wafuatao: Hamza Nkumulwa toka MJUMITA, Ally Namila, Charles Mwaipopo, Abdalla Ndembo, Mussa Mbinga na Manace Nkuli toka Halmashauri ya Wilaya ya Lindi. Pia Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Dar es Salaam kwa kupitia na kupitisha Mpango huu

# YALIYOMO

MUHTASARI WA UTENDAJI ... ii
SHUKRANI ... iii
UTANGULIZI ... viii
SURA YA KWANZA ... 1
1.1 CHIMBUKO ... 1
1.2 MADHUMUNI. ... 1
1.3 UTARATIBU ULIOTUMIKA ... 1
SURA YA PILI ... 2
2.1 Mahali kijiji kilipo na historia. ... 2
2.1.1 Mahali kijiji kilipo ... 2
2.1.2 Historia ya kijiji ... 2
2.2 Maumbile ya Nchi. ... 2
2.2.1 Sura ya nchi na matiririsho ya maji ... 2
2.2.1.1 Sura ya nchi (Physiography) ... 2
2.2.1.2 Matiririsho ya maji ... 2
2.2.2 Hali ya hewa. ... 3
2.2.3 Jiolojia na udongo ... 3
2.2.3.1 Aina za miamba katika kijiji ... 3
2.2.3.2 Aina kuu za udongo ... 3
2.2.4 Uoto ... 4
2.3 RASILIMALI ZA KIJIJI. ... 4
2.3.1 Ardhi. ... 4
2.3.2 Maji ... 5
2.3.2.1 Maji ya mvua ... 5
2.3.2.2 Maji yaliyo juu ya ardhi. ... 5
2.3.2.3 Maji yaliyo chini ya ardhi ... 5
2.3.2.4 Usimamizi wa rasilimali maji ... 5
2.3.2.5 Matumizi ya rasilimali maji. ... 5

2.3.3 Misitu ..... 5
2.3.4 Wanyamapori ..... 6
2.3.5 Madini. ..... 6
2.3.6 Watu na utawala. ..... 6
2.3.6.1 Idadi ya watu kijijini ..... 6
2.3.6.2 Mchanganuo wa kijinsia. ..... 6
2.3.6.3 Uhamaji na uhamiaji ..... 6
2.3.6.4 Makadirio ya idadi ya watu kwa miaka ishirini ijayo. ..... 7
2.3.6.5 Utawala wa kijiji. ..... 7
2.4 HUDUMA ZA JAMII NA MIUNDOMBINU ..... 9
2.4.2 Afya ..... 9
2.4.3 Mawasiliano na uchukuzi. ..... 10
2.4.4 Nishati ..... 10
2.5 MILIKI ZA ARDHI ..... 10
2.5.3 Miliki na usimamizi wa ardhi ..... 10
2.5.4 Upatikanaji wa ardhi. ..... 11
SURA YA TATU ..... 12
3.4 KILIMO. ..... 12
3.4.3 Mazao yanayolimwa. ..... 13
3.4.4 Maeneo ya kilimo na ukubwa wake. ..... 13
3.4.5 Mfumo wa kilimo. ..... 13
3.4.6 Misimu ya kilimo ..... 13
3.4.7 Matumizi ya pembejeo za kilimo ..... 14
3.4.8 Zana za kilimo. ..... 14
3.4.9 Viwango vya uzalishaji ..... 14
3.4.10 Hifadhi ya mazao ..... 15
3.5 UFUGAJI ..... 15
3.5.3 Aina ya mifugo na idadi yake ..... 15
3.5.4 Maeneo ya malisho. ..... 16

3.5.5 Mifumo ya ufugaji ... 16
3.5.6 Magonjwa ya mifugo ... 16
3.5.7 Huduma za miundombinu ya mifugo ... 16
3.6 MISITU / HIFADHI ZA WANYAMAPORI ... 17
3.6.3 Aina na uendelezaji wa misitu ... 17
3.6.4 Matumizi ya misitu na miliki zake. ... 17
3.6.5 Mifumo ya uvunaji wa misitu ... 17
3.7 MAKAZI ... 17
3.7.3 Ukubwa wa eneo la makazi ... 17
3.7.4 Mfumo na aina ya nyumba. ... 18
3.7.5 Vifaa vinavyotumika katika ujenzi na upatikanaji wake. ... 18
3.7.6 Shughuli nyingine ndani ya eneo la makazi. ... 18
SURA YA NNE ... 20
4.1 Matatizo ya kijiji cha Muungano. ... 20
4.2 FURSA ZILIZOPO ... 20
4.3 VIKWAZO VILIVYOPO ... 20
4.4 MIKAKATI YA KUTATUA MATATIZO YA KIJIJI ... 21
4.5 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI KWA USHIRIKISHWAJI JAMII 22
4.5.1 Mpango kazi wa jamii kijiji cha Muungano ... 22
SURA YA TANO ... 24
5.1 UTANGULIZI ... 24
5.2 MAHITAJI HALISI YA ARDHI KWA MATUMIZI MBALIMBALI ... 24
5.2.1 Utangulizi ... 24
5.2.1.1 Mahitaji ya mazao ya chakula ... 25
5.2.1.2 Mahitaji ya zao la biashara ... 25
5.2.2 Mahitaji ya kuni ... 25
5.2.3 Mahitaji ya ardhi kwa ajili ya mifugo ... 25
5.2.4 Mahitaji ya maji kwa ajili ya binadamu. ... 25

5.2.5 Mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo ..... 26
5.2.6 Huduma za kijamii ..... 26
5.3. MAPENDEKEZO ..... 26
5.3.1. Mgawanyo wa ardhi ..... 26
5.3.2 Upimaji wa maeneo ..... 30
5.3.3 Mpango wa kuendeleza maeneo yaliyotengwa. ..... 30
5.3.4 Kazi zitakazofuata. ..... 31

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Aina za udongo na mgawanyo wake kwa vitongoji na matumizi. ..... 3
Jedwali Na 2: Shughuli kuu za kiuchumi ..... 4
Jedwali Na. 3: Uoto wa asili na matumizi yake. ..... 4
Jedwali Na. 4: Idadi ya watu katika kijiji cha muungano kwa jinsia. ..... 6
Jedwali Na. 5: Huduma za jamii na miundombinu ..... 9
Jedwali Na. 6: Umilikaji wa ardhi ..... 10
Jedwali Na. 7: Upatikanaji wa ardhi kwa vitongoji ..... 11
Jedwali Na. 8: Matumizi ya sasa ya ardhi ya kijiji ..... 12
Jedwali Na. 9: Kalenda ya shughuli za kilimo ya kila mwaka ya kijiji cha muungano. ..... 13
Jedwali Na. 10: Uzalishaji wa mazao katika kijiji cha muungano. ..... 14
Jedwali Na.11:Idadi na aina ya mifugo katika kijiji cha Muungano. ..... 16
Jedwali Na. 12: Changamoto, fursa, vikwazo na mikakati ..... 21
Jedwali Na. 13: Mpango kazi wa jamii kijiji cha muungano. ..... 22
Jedwali Na. 14: mapendekezo ya mpango wa matumizi ya ardhi. ..... 27

## ORODHA YA RAMANI

RAMANI MIPAKA YA KIUTAWALA KIJIJI CHA MUUNGANO ..... 8
RAMANI YA KIJIJI CHA MUUNGANO MATUMIZI YA SASA YA ARDHI ..... 19
RAMANI YA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI ..... 29

## VIAMBATISHO

SHERIA NDOGO ZA USIMAMIZI WA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI ZA KIJIJI ..... 32
MUHTASARI YA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MUUNGANO ..... 40

**UTANGULIZI**

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za Ardhi (Sheria ya Ardhi na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na. 5 ya mwaka 1999) kila kijiji hakina budi kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa madhumuni ya kuwezesha usimamizi wa matumzi endelevu ya ardhi na maliasili na rasilimali zake zote. Hatua hii ni muhimu na ya lazima kwa sababu Watanzania walio wengi wanaishi vijijini na shughuli zao za kila siku za kiuchumi na kijamii ndio msingi wa kwanza wa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imebaini kwamba hivi sasa kuna kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji. Kutokana na hali hii, imeandaa mkakati wa Taifa wa kuhifadhi Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika utekelezaji wa Mkakati mojawapo ya nyenzo muhimu zinazotumika kufanikisha malengo yanayohusu jamii ni kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi inayofaa ngazi zote za utawala na usimamizi wa ardhi, ngazi ya kijiji, wilaya, mkoa, kanda, taifa na kimataifa. Kwa ngazi ya kimataifa, Tanzania imeridhia na itaendelea kuridhia Mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusiana na hifadhi ya mazingira ambayo kimsingi ni Mipango ya Kimataifa ya matumizi Bora ya Ardhi. Pia, Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi inakamilisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, na inaendelea na kuandaa pamoja na kuratibu maandalizi ya mipango ya wilaya, mikoa na kanda. Kwa kuwa ngazi ya kijiji ndipo mahali Watanzania wengi wanapoishi na ardhi ndio msingi mkuu wa maendeleo yao. Tume imeweka nguvu ya pekee katika kuwawezesha wanakijiji kuandaa na kurejea mipango ya vijiji vyao.

Tume imejiwekea mkakati wa kuwezesha angalau vijiji 500 kila mwaka katika wilaya mbalimbali. Kazi ambayo inafanyika sawia na kujenga uwezo wa Halmashauri za wilaya husika kwa kuunda timu ya PLUM na kuipatia mafunzo stahiki na kuimarisha taasisi zote za vijiji husika. Pamoja na jitihada za mamlaka nyigine katika kuwawezesha wanakijiji katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vyao, ni matarajio ya Tume kwamba, baada ya muda si mrefu vijiji vyote vya Tanzania Bara; takriban 5130 watakuwa tayari wameandaa mipango yao ya matumizi bora ya ardhi.

Kijiji cha Muungano ni miongoni mwa vijiji ambavyo vimeingizwa katika Wilaya ya Lindi kuwa katika mchakato huu wa kuwasaidia wanakijiji kuandaa na kurejea mipango ya matumizi bora ya Ardhi.

## SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

### 1.1 CHIMBUKO

Kufuata kuwepo kwa kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji, uchakavu wa ardhi, kuongezeka kwa idadi ya watu, ongezeko la mahitaji kwa ajili ya matumizi mbalimbali na ongezeko la migogoro ya ardhi, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Ardhi na Vyanzo vya Maji. Katika kutekeleza mkakati huo, mojawapo ya nyenzo muhimu zinazotumika ni kuhakikisha kunakuwapo na mipango imara ya matumizi bora ya ardhi kwa kila kijiji. Kazi hii inafanyika kwa awamu kutegemea upatikanaji wa fedha na ufadhili; na zamu hii kijiji cha Muungano kimeteuliwa kufanya mpango huu kakika Wilaya ya Lindi kupitia Mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya jamii na uhifadhi wa misitu unaofadhiliwa na Ubalozi wa Norway hapa Tanzania.

### 1.2 MADHUMUNI.

Madhumuni ya utayarishaji wa mipango shirikishi ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kijiji cha Muungano ni kama ifuatavyo:

- Kuelimisha wanakijiji wa kijiji cha Muungano juu ya umuhimu na nafasi ya mipango ya ardhi katika kusimamia rasilimali za pwani na bahari.
- Kubainisha matatizo ya msingi yanayokabili kijiji hicho na fursa/nafasi waliyonayo wanakijiji kuweza kutatua matatizo hayo.
- Kutoa elimu kuhusu sheria ya Ardhi ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na sheria ya matumizi ya ardhi.
- Kutayarisha mipango ya awali ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kuzingatia matakwa ya jamii (umma na watu binafsi)
- Kuwawezesha wanakijiji kukubaliana aina mbalimbali za matumizi ya Ardhi na kuzitengea maeneo, kuyapima na kuyaingiza kwenye ramani.
- Kutunga sheria ndogo za kutekelea makubaliano mbalimbali ya matumizi ya Ardhi.
- Kupitishwa mpango wa matumizi ya ardhi na sheria ndogo na mkutano wa kijiji

### 1.3 UTARATIBU ULIOTUMIKA

Hatua muhimu zilizofuatwa katika zoezi hili ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukusanya na kuchambua takwimu muhimu za kijiji
(ii) Kubainisha matatizo ya msingi ya kijiji
(iii) Kutayarisha mpango kazi wa jamii
(iv) Kutayarisha mikakati ya kutatua matatizo yaliyobainishwa.
(v) Kutayarisha mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi wa kijiji
(vi) Kutayarisha sheria ndogo
(vii) Kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji
(viii) Kupima maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kuyaingiza kwenye ramani ya kijiji
(ix) Kuandaa rasimu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji na aramani
(x) Kuwasilisha mpango kwenye Halmashauri ya Wilaya ili upitishwe
(xi) Kuwawasilisha mpango TUME

# SURA YA PILI

## 2. TAARIFA ZA MSINGI ZA KIJIJI

### 2.1 Mahali kijiji kilipo na historia

#### 2.1.1 Mahali kijiji kilipo

Kijiji cha Muungano kipo katika Kata ya Nangaru, Tarafa ya Nangaru katika Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi, eneo lake lipo kati ya jira 8904029 na 8918061 kaskazini na 537910 na 551306 mashariki (Datum WGS 84). Kijiji cha Muungano ni miongoni mwa vijiji 134 vya Wilaya ya Lindi.

Kijiji hiki ni cha asili na kipo umbali wa kilometa 55 kutoka makao makuu ya Wilaya, mwishoni mwa barabara itokayo Mtange kwenda Nangaru. Kipo katika kata ya Nangaru, Tarafa ya Nangaru, Wilaya ya Lindi. Kimepakana na kijiji cha Mkombamosi kwa upande wa Mashariki na kwa upande wa Magharibi kijiji kimepakana na Kiwawa, kwa upande wa kusini kijiji kimepakana na kijiji cha Ruhoma na Milola magharibi na kwa upande wa Kaskazini kijiji kimepakana na Namkongo na Lihimilo. Kijiji kina ukubwa wa hekta 10,479.00 sawa na kilomita za mraba 104.79.

#### 2.1.2 Historia ya kijiji

Hapo mwanzo eneo hili lilikuwa na vijiji vidogo vya Uleka, Michee, Kipunga, Likonde, Likandilo, Mkombamosi, Makumba, Noto, Likonde la pili, Mtonya na Lumo. B na kufikia mwaka 1954 vijiji hivi viliungana na kujulukana kama kijiji cha Nangaru. Jina la Nangaru lilitokana na jina la Mzee mmoja aliyeitwa Nangaru. Ilipofika mwaka 1956 kijiji kilitenganishwa na kuwa vijiji viwili vya Mkombamosi na Muungano chenye vitongoji saba. Jina la Mkombamosi lilitokana na jina la kitongoji cha Mkombamosi.

Mwaka 1974 wakati wa operation vijiji kijiji cha Muungano kilianzanhatua ya kuwa kijiji kamili na kupat cheti cha kijiji mwaka 1976

### 2.2 Maumbile ya Nchi.

#### 2.2.1 Sura ya nchi na matiririsho ya maji

##### 2.2.1.1 Sura ya nchi (Physiography)

Maumbile ya kijiji cha Muungano yamegawanyika katika makundi yafuatayo:- Tambarare, milima, mabonde na vijito. Maeneo mengi ya tambarare yanatumika kwa ajili ya kilimo na makazi wakati maeneo ya mabonde yanatumika kwa kilimo.

##### 2.2.1.2 Matiririsho ya maji

Katika kijiji cha Muungano mtiririko wa maji yote ya mvua na vijito inakwenda katika bahari ya Hindi.

### 2.2.2 Hali ya hewa

Hali ya hewa ya kijiji cha Muungano inafanana na hali ya hewa ya Wilaya ya Lindi vijijini katika vijiji vya Pwani ambapo kuna mvua za wastani wa mvua ni milimeta 750 hadi 1000 kwa mwaka. Kuna misimu miwili ya mvua, mvua za vuli na mvua za masika. Mvua za vuli huanza mwezi Novemba hadi Januari na vua za masika huanza mwezi Machi hadi Mei. Mwezi wa Juni hadi Julai ni majira ya baridi baada ya hapo mwezi Agosti hadi Novemba ni majira ya joto. Wastani wa hali joto kwa mwaka ni wastani wa sentigredi 24.0 na 28. Wastani wa unyevu katika hewa kila siku kwa mwaka ni asilimia 88. Kiwango cha mvua huzidi mvukizo mwezi Machi na Aprili na hiki ndicho kipindi cha kuandaa mashamba.

### 2.2.3 Jiolojia na udongo

#### 2.2.3.1 Aina za miamba katika kijiji

Miamba aina ya Jurasiki yenye mawe ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mawe, mchanga na gypsum imetawala katika kijiji cha Muungano maeneo ya Noto.

#### 2.2.3.2 Aina kuu za udongo

Aina ya udongo katika kijiji ni udongo wa *Feralic combrisols* ambao ni udongo mweusi uliochanganyika na mchanga kiasi na wenye rutuba na ambao haupitishi maji kwa haraka. Tabaka la chini la udongo huu ni mfinyazi. Katika maeneo ya mabonde aina hii ya udongo wa mfinyanzi umejitokeza juu. Katika maeneo ya mwinuko yaliyofunikwa na miti udongo kiasi cha mfinyanzi kimeongezeka na kufanya udongo tifutifu mwekundu weye rutuba ya asili.

**Jedwali Na. 1: Aina za udongo na Mgawanyo wake kwa vitongoji na matumizi**.

| Aina ya udongo | En eo | Asilimia ya kijiji | Kiwango cha rutuba | Mazao yanayostawi zaidi | Vikwazo | Vitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Udongo mweusi na tifutifu | | 70% | Yakutosha | Mahindi Mtama Ufuta Mpunga | Sisimizi Magugu | Kipunga, Uleka,Naruwi, Likonde juu, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa |
| Udongo mwekundu | | 20% | Yakutosha | Muhogo, minazi mtama, korosho migomba na karanga | Mchwa mzito hunata | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka |
| Mfinyanzi | | 10% | Nyingi | Mtama, Mpunga, Mahindi, Ufuta Na Nazi | Kutohamisha udongo mgumu, mzito Maji kutuama | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

**Jedwali Na 2: Shughuli kuu za kiuchumi**

| Kitongoji | Kilimo % | Ufugaji % | Wengine % | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kipunga | 90 | 6 | 4 | 100 |
| Uleka | 90 | 5 | 5 | 100 |
| Naruwi | 90 | 10 | 0 | 100 |
| Likonde juu | 95 | 5 | 0 | 100 |
| Mnazi mmoja | 85 | 5 | 10 | 100 |
| Umoja | 86 | 4 | 10 | 100 |
| Ujamaa | 83 | 7 | 10 | 100 |
| **WASTANI** | **88.4** | **6** | **5.6** | **100** |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na Mikutano ya vitongoji, 2011**

### 2.2.4 Uoto

Kijiji cha Muungano kimefunikwa kwa kiasi kikubwa na misitu ya miombo na misitu ya pwani kwa sehemu ndogo pamoja na vichaka na nyasi. Hata hivyo misitu hii imekuwa ikipungua kutokana na ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya upanuzi wa mashamba na mahitaji ya majengo na mbao. Upo pia uoto wa kupandwa ingawa kiasi ni kidogo ukilinganisha na uoto wa asili. Uoto huu umetawaliwa na mikorosho na minazi mashambani na katika maeneo ya makazi. Upandaji miti unafanyika pia katika maeneo ya taasisi kama vile shule. Aina mbalimbali za uoto na matumizi yake zimeanishwa katika jedwali hapo chini.

**Jedwali Na. 3: Uoto wa asili na matumizi yake.**

| Na | Aina ya uoto | % eneo la kijiji | Vitongoji | Aina ya miti | Matumizi ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Misitu | 60% | Likonde juu, Kipunga, Ujamaa, Naruwi, Uleka | Mmalala Mtumbati Msufi pori, | Mbao, Uchongaji wa vinu na Matambiko |
| 2 | Vichaka na miti | 25% | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | Mmalala Mtumbati, Msufi pori, Mng'epukano | Kilimo, Miti ya ujenzi, Makazi ya wanyama na malisho (mbawala, ng'ombe) Mifugo |
| 3 | Vichaka na nyasi | 15% | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | Mshazi, Mmalala Muhiadi | - Kilimo |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

## 2.3 RASILIMALI ZA KIJIJI.

### 2.3.1 Ardhi.

Katika kijiji cha Muungano mojawapo ya raslimali iliyopo ni ardhi ya kijiji. Ardhi ya kijiji ina ukubwa wa ha 10,479.00; kati ya hizo ha 760.95 zinafaa kwa shughuli za kilimo 4201.58ha inafaa kwa makazi ha 5514.99 kwa msitu wa hifadhi wa kijiji. Eneo liliobaki linafaa kwa matumizi mengine ya baadaye kama uwezekezaji wa aina yeyote.

### 2.3.2 Maji

Rasilimali ya maji iliyopo katika kijiji cha Muungano ni pamoja na mvua, mito na vijito vidogo, vyanzo vya maji vya mto Muungano. Kijiji cha Muungano kinapata maji baridi ya kutosha kwa ajili ya matumizi yao kwani kuna mabomba yanayotoa maji baridi kutoka vyanzo vya maji vya mto milola, pia mto milola na mto Muungano inatiiririsha maji mwaka mzima.

#### 2.3.2.1 Maji ya mvua

Katika kijiji cha Muungano kiasi cha maji ya mvua kwa mwaka hakijulikani. Aidha, mzunguko wa maji haya ni kama ufuatao: kiasi huzama ardhini na huvuja mpaka kwenye vilindo vya maji chini ya ardhi na kusheheneza limbiko la maji ya chini ya ardhi, maji mengine hurudi katika anga hewa kupitia mchakato wa mvukizo, moja kwa moja au kupitia kwenye uoto na maji mengine hubaki juu ya ardhi katika mito.

#### 2.3.2.2 Maji yaliyo juu ya ardhi.

Katika kijiji cha Muungano maji yaliyo juu ya ardhi yapo katika mto Milola na Muungano ambapo vijito vingine huanzia. Hata hivyo vijito vingi hukauka wakati wa kiangazi. Wingi wa maji haya haufahamiki kutokana na kutokuwepo na utaratibu wa upimaji wa kihaidrojia na kihaidrolojiolojia

#### 2.3.2.3 Maji yaliyo chini ya ardhi

Kwa mujibu wa tafiti za kijiolojia, na kihairolojia, ukanda kilipo kijiji cha Muungano bado haifahamiki kiasi cha maji yaliyopo chini ya ardhi.

#### 2.3.2.4 Usimamizi wa rasilimali maji

Katika kijiji cha Muungano, licha ya kutokuwepo shughuli za upimaji maji kihaidrolojia na kihaidrolojiolojia. Kama vile vipimo vya mvua, wingi na kina cha maji yaliyo juu ya ardhi na kina cha maji yaliyo chini ya ardhi kutoka kwenye uso wa ardhi. Kijiji cha Muungano tayari kimeunda kamati ya maji na tayari wameanzisha mfuko wa maji.

#### 2.3.2.5 Matumizi ya rasilimali maji.

Matumizi makuu ya maji katika kijiji cha Muungano ni pamoja na matumizi ya kawaida ya nyumbani ikiwa ni pamoja na kunywa, kupikia, kufulia, kujengea, pia kumwagilia bustani za mboga wakati wa kiangazi.

### 2.3.3 Misitu

Katika kijiji cha Muungano uoto wa asili unapungua hususani miti, kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kijijini. Hivi sasa pamoja na kilimo cha kuhamahama, ukataji holela wa miti kwa ajili ya mbao na majengo unaendelea. Uoto huu unaweza kutoweka iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa kusimamia utunzaji wa uoto huu. Uoto wa asili uliopo unajumuisha aina mbalimbali za miti ambazo ni pamoja na mtumbati, mchenga, mibuyu, Mmalala, Mchinji, Mnjembe, Mchiu, Msufipori na mtanga.

### 2.3.4 Wanyamapori

Katika kijiji cha Muungano kuna wanyama pori wengi hii ni kutokana na kuwepo kwa misitu minene ya Noto, Makuani, Machaninga na Likonde juu ambayo ni makazi ya wanyama hao. Wanyama waliopo ni pamoja na Simba, Chui, Tembo, Nyani, Ng'onde, Digidigi na Nguruwe.

### 2.3.5 Madini.

Katika kijiji cha Muungano uchunguzi juu ya kuwepo kwa madini bado haujafanyika hivyo bado haijulikani kama kuna aina yeyote ya madini kijijini.

### 2.3.6 Watu na utawala.

#### 2.3.6.1 Idadi ya watu kijijini

Katika kijiji cha Muungano idadi ya watu ni 2471 ambao wanaume 1013 na wanawake ni 1458 idadi ya kaya ni 650

#### 2.3.6.2 Mchanganuo wa kijinsia.

Idadi kwa jinsia ya watu katika kijiji cha Muungano ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 4.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya watu katika kijiji cha Muungano kwa jinsia.**

| Kitongoji | Me | Ke | Watoto | | Jumla | Kaya |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | | |
| Kipunga | 241 | 270 | 96 | 100 | 707 | 260 |
| Uleka | 96 | 187 | 56 | 83 | 422 | 60 |
| Naruwi | 56 | 64 | 35 | 42 | 197 | 50 |
| Likondu juu | 48 | 52 | 18 | 28 | 146 | 90 |
| Mnazi mmoja | 56 | 230 | 118 | 140 | 544 | 70 |
| Umoja | 53 | 82 | 56 | 66 | 257 | 55 |
| Ujamaa | 53 | 66 | 31 | 48 | 198 | 65 |
| **Jumla** | **603** | **951** | **410** | **507** | **2471** | **650** |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

#### 2.3.6.3 Uhamaji na uhamiaji

Tathimini ya timu ya PLUM ya wilaya na wataalamu MKUHUMI kwa kushirikiana na VLUM na serikali ya kijiji inaonyesha kuwa wenyeji ni asilimia 94 na idadi kubwa ya wanakijiji ni wa asili. Kuhusu uhamaji na uhamiaji kijijini, kutokana na maelezo ya Halmashauri ya kijiji, kuna wanakijiji ambao kwa sababu mbalimbali huwa wanaamua kuhama kwenda kuishi kwenye maeneo mengine katika vijiji vingine au mijini ndani ya wilaya au sehemu nyingine za nchi, pia watu wanaohamia kijijini kutoka vijiji vingine au sehemu nyingine za nchi ni wachache sana. Hata hivyo hakuna taarifa rasmi juu ya wahamaji na wahamiaji.

#### 2.3.6.4 Makadirio ya idadi ya watu kwa miaka ishirini ijayo.

Makadirio ya idadi ya watu katika kipindi cha miaka ishirini ijayo, takwimu zinaonyesha kuwa Novemba 2012 kijiji kina watu 2471 ambao 1013 ni wanaume na wanawake 1458, na idadi ya kaya ni 650 kwa mujibu wa sensa ya taifa ya mwaka 2002 ongezeko la idadi ya watu katika wilaya ni asilimia 1.3 kwa hiyo, ifikapo mwaka 2031 (baada ya kipindi cha miaka ishirini) inakadriwa kwamba idadi ya watu katika kijiji itakuwa 3083 na kaya zitakuwa ni 771.

#### 2.3.6.5 Utawala wa kijiji.

Kijiji kina serikali ambayo ina wajumbe 25. Serikali hiyo ambayo huchaguliwa kila baada ya miaka 5 kazi yake kubwa ni kusimamia shughuli zote za kijiji zikiwemo shughuli za maendeleo na kijamii. Ili kutekeleza majukumu, Serikali ya kijiji imejipanga katika kamati tatu za kudumu nazo ni:-


- Kamati ya uchumi na fedha
- Kamati ya huduma za jamii
- Kamati ya Ulinzi na usalama

Aidha, Serikali ya kijiji imeunda kamati/timu za kusimamia majukumu mbalimbali, timu hizo kimsingi sio za kudumu bali uundwa kwa ajili ya kukidhi haja fulani ambazo zaweza kuwa za muda. Kamati/timu hizo ni pamoja na:-

- Timu ya matumizi bora ya ardhi (VLUM)
- Baraza la ardhi ya kijiji
- Kamati ya maji
- Kamati ya Maliasili ikiwa ni pamoja na msitu wa hifadhi wa kijiji (kupitia MKUHUMI)

Kijiji kwa sasa kinajenga ofisi mpya ikishirikiana mradi wa Mkuhumi.

RAMANI YA KIJIJI CHA MUUNGANO KUONYESHA MAHALI KILIPO



## 2.4 HUDUMA ZA JAMII NA MIUNDOMBINU

Huduma za jamii zilizopo ni shule ya msingi Muungano ambayo ndo kwanza inaanza kujengwa, msikiti, maduka, soko, ofisi ya CCM, ghala na mabomba ya maji, mganga wa jadi, mashine ya kusaga, uwanja wa unyago, fundi selemala na fundi cherehani. Ipo barabara inayoanzia Nangaru - Muungano kwenda Lindi kupitia kata za Matimba, Chikonji hadi Mtange, barabara kuu ya Lindi Mtwara. Mawasiliano ya simu ni imara kutokana na kuwepo kwa Mnara wa simu wa Airtel katika miinuko ya Noto na mwingine hapo kijijini. Huduma za jamii zimegawanyika katika kila kitongoji kama ilivyo kwenye jedwali Na. 5

**Jedwali Na. 5: Huduma za jamii na miundombinu**

| Kitongoji | Huduma za Jamii na Miundombinu |
|---|---|
| Kipunga | Msikiti,Mganga wa Jadi, Vioski, Barabara, Fundi seremala, Fundi cherehani, Fundi do do do na Uwanja wa Unyago |
| Uleka | Kituo cha Elimu,Kilabu cha pombe, Mashine ya Kusaga, Vioski, Mganga wa Jadi, Uwanja wa Unyago, Fundi seremala na Fundi Cherehani |
| Naruwi | Fundi mwashi na Mnara wa simu wa Noto |
| Likonde juu | Msikiti, Mganga wa Jadi na Uwanja wa Unyago |
| Mnazi mmoja | Mashine ya Kusaga, Kilabu cha pombe, Barabara, Ofisi ya kijiji na Mganga wa Jadi |
| Umoja | Uwanja wa Unyago, Kioski,Mnara wa Simu, Barabara,Mganga wa Jadi |
| Ujamaa | Barabara, Mashine ya Kusaga, Fundi cherehani, vioski, Mgahawa, Fundi seremala, Ghala, Makaburi na Kilabu cha pombe |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

### 2.4.1 Elimu

Kwa upande wa elimu kijiji cha Muungano kinatumia shule iliyopo katika kijiji cha Mkombamosi ambapo familia za watoto wengi walioko mbali na shule hii hawapati huduma hii. Shule ya kijiji cha Muungano ndo inaanza kujengwa ambapo itatumika na wakazi wote wa kijijini hapa.

### 2.4.2 Afya

Na kwa upande wa afya kijiji cha Muungano hakina zahanati ya kijiji, hivyo kinategemea zaidi zahanati ya kata iliyojengwa katika kijiji cha Mkombamosi. Wakazi wengi wa Muungano wamejenga vyoo, hivyo kufanya kuwepo kwa usafi na kupunguza magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

### 2.4.3 Mawasiliano na uchukuzi.

Katika kijiji cha Muungano kuna barabara moja tu inayotambulika na kupitika muda wote inayotoka barabara kubwa ya kwenda Lindi – Mtwara na kwenda kijiji cha Muungano. Pia, barabara / njia zisizo rasmi na zinazounganisha vitongoji na vijiji jirani zinapitika kwa shida kwa gari hivyo zinahitaji kuboreshwa.

Katika kijiji cha Muungano mtandao wa simu unaopatikana ni Airtel ambapo ipo minara miwili ya mtandao huu mmoja ukiwa kwenye miinuko ya Noto na mwingine hapa kijijini, hivyo mawasiliano kwa mtandao wa Airtel yanapatikana maeneo yote kijijini.

### 2.4.4 Nishati

Tegemeo kubwa la nishati za asili katika kijiji hiki ni kuni. Aina nyingine ya nishati za asili zilizopo ni nguvu ya joto la jua na nguvu za upepo ambazo hata hivyo hazitumiki kikamilifu. Mathalani nguvu ya joto la jua hutumika sana kwa kukaushia mazao na nguo wakati ingeweza pia kuzalisha umeme. Nishati ya upepo ingeweza kusaidia kusukuma maji kutoka chini ya ardhi kwa matumizi ya nyumbani, wanyama na bustani. Tegemezi ya nishati ya kuni inafanya misitu kuwa raslimali muhimu sana kijijini.

## 2.5 MILIKI ZA ARDHI

### 2.5.3 Miliki na usimamizi wa ardhi

Miliki za ardhi katika kijiji cha Muungano ni za kimila. Sehemu kubwa ya kijiji, eneo la mashamba makazi linamilikiwa na familia mojamoja au mtu mmoja mmoja. Sehemu kubwa ya eneo la Misitu na mapori inamilikiwa kijumuia chini ya usimamizi na uangalizi wa serikali ya kijiji. Maeneo ya matumizi ya jumla ambayo ni pamoja na maeneo ya shule, soko, msikiti na ghala yapo chini ya serikali ya kijiji.

**Jedwali No. 6: Umilikaji wa Ardhi**

| Kitongoji | Wanaomiliki % | Wanaokodi % | Wengine | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kipunga | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Uleka | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Naruwi | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Likonde juu | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Mnazi mmoja | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Umoja | 100 | 0 | 0 | 100 |
| Ujamaa | 100 | 0 | 0 | 100 |
| **Wastani** | 100 | **0** | **0** | **100** |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

### 2.5.4 Upatikanaji wa ardhi.

Watu wengi wamepata ardhi kwa kurithi kutoka kwa wazazi wao. Wastani wa ukubwa wa eneo la shamba ni ekari 4 kwa kila kaya. Aidha, familia zinazomiliki ardhi kwa kurithi ni 75% kwa kununua ni asilimia 22% na kugawiwa ni asilimia 1%, wanaopata kwa njia nyinginezo ikiwemo kuvamia maeneo ya kijiji ni 2%. Angalia jedwali namba 7 – Upatikanaji wa ardhi kwa Vitongoji.

**Jedwali Na. 7: upatikanaji wa ardhi kwa vitongoji**

| Kitongoji | Kugawiwa % | Kurithi % | Kununua % | Wengine % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Kipunga | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Uleka | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Naruwi | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Likonde juu | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Mnazi mmoja | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Umoja | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| Ujamaa | 1 | 75 | 22 | 2 | 100 |
| **Wastani** | **1** | **75** | **22** | **2** | 100 |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

## SURA YA TATU

## 3 MATUMIZI YA ARDHI YA SASA.

Katika kijiji cha Muungano matumizi ya ardhi yaliyopo ni pamoja na Kilimo, Makazi, Ufugaji, Uvunaji wa mazao ya misitu, huduma za jamii na miundo mbinu (barabara, shule na huduma za jamii na kiuchumi). Jedwali lifuatalo linaonyesha matumizi ya ardhi ya sasa katika kijiji cha Muungano.

**Jedwali Na. 8: Matumizi ya sasa ya ardhi ya kijiji**

| Na | Aina ya mtumizi | % ya kaya zinazojihusisha | Mahali inapofanyika kijijini | Vitongoji husika | % ya kijiji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilimo | 100% | Eneo la tambarale na mwinuko | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | 45% |
| 2 | Makazi | 100% | Vitongoji vyote | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | 25% |
| 3 | Makazi/Kilimo | 25% | Vitongoji vyote | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | 25% |
| 5 | Uvunaji wa mazao ya misitu (Mkaa, Mbao na Boriti) | 5% | Msitu wa Noto na Likonde juu | Likonde juu, Kipunga, Mnazi mmoja, Umoja, Ujamaa, Naruwi, Uleka | 5% |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

## 3.4 KILIMO.

Kilimo ni shughuli kuu ya kiuchumi na kijamii inayotegemewa na watu. Tathimini iliyofanywa na timu ya PLUM na wataalamu wa MKUHUMI kwa kushirikiana na Halmashaui ya kijiji inaonyesha kwamba asilimia kubwa ya wanakijiji ni wakulima ambao wengi wao hulima mashamba ya kudumu ya mazao ya korosho na minazi na kila kaya hulima mazao ya chakula na biashara kwenye mashamba ya muda kwa mtindo wa kuhamahama.

### 3.4.3 Mazao yanayolimwa.

Mazao ya chakula ni mahindi, mpunga, mtama, mihogo, kunde na mbaazi, njugu, karanga na migomba. Mazao ya biashara ni ufuta, korosho na nazi. Mazao ya ufuta, nazi na mbaazi hulimwa pia kama mazao ya biashara na chakula.

### 3.4.4 Maeneo ya kilimo na ukubwa wake.

Kwa ujumla ardhi ya kijiji cha Muungano ina Ukubwa wa jumla ya hekta 10,479.00 sawa na kilomita za mraba 104.79 ambapo kilimo kwa pekee yake ni ha 760.95. Eneo la makazi mashamba lina Ukubwa wa ha 3622.75 na eneo la makazi msongamano ni ha 578.83.

### 3.4.5 Mfumo wa kilimo.

Mfumo wa kilimo unaotumika Muungano ni kilimo cha mseto kwa mazao yote. Kilimo hiki ni matokeo ya ulimaji wa maeneo madogo na matumizi ya zana duni za kilimo likiwemo jembe la mkono. Huduma ya ugani hupatikana kutoka kwa maofisa ugani waliopo katani. Wanakijiji walio wengi huhifadhi mazao katika makese, viroba, magunia na darini. Ghala linahifadhi mazao ya biashara hasa korosho.

### 3.4.6 Misimu ya kilimo

Katika kijiji cha Muungano majira ya kilimo ni kama yalivyoainishwa katika jedwali Na. 9 hapo chini.

**Jedwali Na. 9: kalenda ya shughuli za kilimo ya kila mwaka ya kijiji cha Muungano**.

| Na | Shughuli | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuandaa mashamba | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Kulima mashamba | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kupanda | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Kupalilia | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Kulinda wanyama | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Kuvuna | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Kuhifadhi mazao | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Kula na kuuza | | | | | | | | | | | | |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na Mikutano ya Vitongoji, 2011**

### 3.4.7 Matumizi ya pembejeo za kilimo

Ukosefu wa pembejeo ni tatizo linalowakabili wanakijiji wa kijiji cha Muungano. Hata hivyo baadhi ya pembejeo zinapatikana kijijini ila wanakijijini wengi hawana uwezo wa kununua. Hivyo kufanya watumiaji wa pembejeo za kilimo kuwa wachache.

### 3.4.8 Zana za kilimo.

Jembe la mkono ndilo linaloongoza kuwa na watumiaji wengi zaidi. Matumizi ya zana zingine kama matumizi ya *power tiller* (trekta la mkono) hutumiwa na wachache wenye uwezo wa kulipa gharama hizo.

### 3.4.9 Viwango vya uzalishaji

Kwa ujumla uzalishaji wa mazao na hasa mazao ya chakula ni mdogo ukilinganisha na mahitaji ya kaya kwa mwaka. Jedwali Na. 10 linaonyesha wastani wa uzalishaji wa kila zao kwa mwaka na kwa kila hekari.

**Jedwali Na. 10: uzalishaji wa mazao katika kijiji cha Muungano.**

| Kitongoji | Zao | Wastani wa ekari kwa kaya | Uzalishaji kwa ekari (Gunia) | Jumla ya kaya | Jumla ya ekari | Mazao kwa mwaka (Gunia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kipunga** | **Mahindi** | **2** | **6** | **110** | **220** | **1320** |
| | **Mtama** | **1** | **3** | **110** | **110** | **330** |
| | **Mpunga** | **2** | **6** | **15** | **30** | **180** |
| | **Muhogo** | **1** | **10** | **195** | **195** | **1950** |
| | **Ufuta** | **1** | **5** | **50** | **50** | **250** |
| | **Nazi** | **2** | **3** | **6** | **12** | **36** |
| | **Korosho** | **1** | **3** | **110** | **110** | **330** |
| **Uleka** | **Mahindi** | **2** | **4** | **60** | **120** | **480** |
| | **Mtama** | **2** | **4** | **45** | **90** | **360** |
| | **Mpunga** | **3** | **3** | **30** | **90** | **360** |
| | **Muhogo** | **0.5** | **1** | **15** | **7.5** | **7.5** |
| | **Ufuta** | **2** | **3** | **60** | **120** | **360** |
| | **Nazi** | **1** | **8** | **15** | **15** | **120** |
| | **Korosho** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Naruwi** | **Mahindi** | **2** | **4** | **50** | **100** | **400** |
| | **Mtama** | **2** | **3** | **50** | **100** | **300** |
| | **Mpunga** | **2** | **3** | **25** | **50** | **150** |
| | **Muhogo** | **0.5** | **1** | **13** | **6.5** | **6.5** |
| | **Ufuta** | **2** | **3** | **50** | **6.5** | **300** |
| | **Nazi** | **0.5** | **8** | **13** | **6.5** | **52** |
| | **Korosho** | **0.5** | **1** | **13** | **6.5** | **6.5** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Likonde juu** | **Mahindi** | **3** | **4** | **90** | **270** | **108** |
| | **Mtama** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| | **Mpunga** | **3** | **2** | **4.5** | **135** | **270** |
| | **Muhogo** | **2** | **5** | **90** | **180** | **900** |
| | **Ufuta** | **1** | **2** | **45** | **45** | **90** |
| | **Nazi** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| | **Korosho** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Mnazi mmoja** | **Mahindi** | **3** | **3** | **70** | **210** | **630** |
| | **Mtama** | **2** | **3** | **35** | **70** | **210** |
| | **Mpunga** | **2** | **4** | **18** | **36** | **144** |
| | **Muhogo** | **0.5** | **1** | **18** | **9** | **9** |
| | **Ufuta** | **2** | **3** | **53** | **106** | **318** |
| | **Nazi** | **0.5** | **8** | **35** | **18** | **144** |
| | **Korosho** | **0.5** | **1** | **18** | **9** | **9** |
| **Umoja** | **Mahindi** | **2** | **3** | **55** | **110** | **330** |
| | **Mtama** | **2** | **3** | **26** | **52** | **156** |
| | **Mpunga** | **2** | **4** | **26** | **52** | **208** |
| | **Muhogo** | **0.5** | **1** | **13** | **6.5** | **6.5** |
| | **Ufuta** | **2** | **3** | **39** | **78** | **234** |
| | **Nazi** | **0.5** | **8** | **13** | **6.5** | **52** |
| | **Korosho** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Ujamaa** | **Mahindi** | **3** | **4** | **65** | **195** | **780** |
| | **Mtama** | **4** | **4** | **33** | **132** | **528** |
| | **Mpunga** | **0.25** | **3** | **17** | **4.25** | **25.75** |
| | **Muhogo** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| | **Ufuta** | **2** | **3** | **50** | **100** | **300** |
| | **Nazi** | **0.5** | **8** | **17** | **8.5** | **68** |
| | **Korosho** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na mikutano ya vitongoji, 2011**

### 3.4.10 Hifadhi ya mazao

Kutokana na riporti zilizopatikana katika kijiji cha Muungano, wanakijiji walio wengi huhifadhi mazao katika makese, viroba/maguni na darini. Hata hivyo ilidhihirisha kuwa upatikanaji wa viroba na magunia ni mgumu kidogo kutokana na umbali wa vifaa hivyo vilipo.

## 3.5 UFUGAJI

### 3.5.3 Aina ya mifugo na idadi yake

Mifugo iliyopo ni Mbuzi, kuku na Bata. Hata hivyo kuku ndio mifugo ambayo inawakimu wanakijiji wa Muungano ambapo hutumiwa kama kitoweo na kuuzwa. Takwimu za mifugo zimeonyeshwa kwenye jendwali Na. 11

**Jedwali Na. 11: Idadi na aina ya mifugo katika kijiji cha Muungano**

| Kitongoji | Ng'ombe | Mbuzi | Kondoo | Bata | Kuku |
|---|---|---|---|---|---|
| Kipunga | 0 | 100 | 0 | 0 | 1040 |
| Uleka | 0 | 43 | 0 | 0 | 240 |
| Naruwi | 0 | 31 | 0 | 3 | 200 |
| Likonde juu | 0 | 0 | 0 | 0 | 360 |
| Mnazi mmoja | 0 | 33 | 0 | 0 | 280 |
| Umoja | 0 | 14 | 0 | 6 | 220 |
| Ujamaa | 0 | 100 | 0 | 0 | 260 |
| **Jumla** | **0** | **321** | **0** | **9** | **2,600** |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na kamati ya matumizi bora ya ardhi (VLUM), 2011**

### 3.5.4 Maeneo ya malisho.

Hakuna eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya malisho na kuchungia mifugo, pia hakuna njia maalum za mifugo. Wakati mwingine hali hii husababisha mifugo kuingia mashambani na kula mazao hivyo kusababisha migogoro isiyo ya lazima. Aidha, kutokana na hali hii wakulima hulazimika kulisha mifugo yao kandokando ya makazi na kunyweshea kwenye ndoo na mabeseni kwa kutumia maji ya mvua au yaliochotwa visimani.

### 3.5.5 Mifumo ya ufugaji

Katika kijiji cha Muungano mifugo iliyopo hufungiwa majumbani lakini wengine huachia mifugo yao kuzunguka kijijini.

### 3.5.6 Magonjwa ya mifugo

Magonjwa ya mifugo yaliyopo kijijini hapa:- kuku ugonjwa mkubwa ni mdondo na kideli, kwa upande wa mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo magonjwa makuu ni homa ya mapafu, minyoo na kuhara.

### 3.5.7 Huduma za miundombinu ya mifugo

Kutokana na kutokuwepo kwa maeneo ya mnada wa mifugo, wafugaji hawana uhuru wa kuuza mifugo yao na hulazimika kuuza kwa bei ndogo kutokana na kutokuwepo kwa maeneo maalum ya kuuzia mifugo na mazao yake. Pia kijiji hiki kinakabiliwa na ukosefu wa njia maalum za kupitishia mifugo. Wakati mwingine hali hii husababisha mifugo kuingia mashambani na kula mazao hivyo kusababisha migogoro isiyo ya lazima. Aidha, kutokana na kutokuwepo kwa lambo la kunyweshea mifugo wafugaji wanalazimika kunyweshea mifugo yao kwenye ndoo na mabeseni kwa kutumia maji ya mvua au yaliochotwa visimani. Kijiji cha Muungano hakina mtaalamu wa mifugo, kwa hivyo inakuwa ni tatizo kupata ushauri kwa wafugaji kijijini.

## 3.6 MISITU / HIFADHI ZA WANYAMAPORI

### 3.6.3 Aina na uendelezaji wa misitu

Katika kijiji cha Muungano kuna misitu mizuri ya asili hasa sehemu za Noto lakini inapungua hususani miti, kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika kijijini. Hivi sasa pamoja na kilimo cha kuhamahama, ukataji holela wa miti kwa ajili ya mbao, kujengea hufanya miti kupungua siku hadi siku. Misitu hii inaweza kutoweka iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa kusimamia utunzaji wa uoto huu. Uoto wa asili uliopo unajumuisha aina mbalimbali za miti ambazo ni mtumbati, mchenga, mibuyu, Mmalala, Mchinji, Mnjembe, Mchiu, Msufipori na mtanga

Jitihada za uendelezaji wa rasilimali ya misitu katika kijiji cha Muungano umekuwa siyo za kuridhisha. Hali hii inatokana na kijiji kuwa bado na maeneo makubwa ya misitu. Halmashauri ya kijiji na wanakijiji kwa ujumla wameupokea Mradi wa MKUHUMI kama njia ya utunzaji endelevu wa misitu, pia kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Mradi wa MKUHUMI utasaidia kijiji kupata fedha za malipo ya Hewa ya Ukaa kutokana na utunzaji wa msitu. Aidha, katika kijiji tayari kuna kamati ya Maliasili inayosimamia mazingira pamoja na misitu.

### 3.6.4 Matumizi ya misitu na miliki zake.

Katika kijiji cha Muungano matumizi makubwa ya mazao ya misitu katika kijiji ni pamoja na kuni, mijengo (nyasi na miti), mbao, dawa za miti shamba, uchongaji wa vinu, malisho ya mifugo, matambiko, makazi ya wanyama. Misitu yote iliyopo kijijini husimamiwa na Halmashauri ya kijiji kupitia Kamati ya Maliasili.

### 3.6.5 Mifumo ya uvunaji wa misitu

Kwa ujumla, mfumo wa uvunaji wa misitu katika kijiji cha Muungano ni holela ambapo hakuna eneo la misitu ambalo limetengwa kwa ajili ya hifadhi na matumizi ya kijiji. Hivyo hali hii inapelekea maeneo mengi ya msitu kuvamiwa na kukatwa ovyo. Hivyo ni muhimu zaidi kwa kijiji kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kunusuru kuteketea kwa uoto huo wa asili pamoja na kutekeleza mradi wa MKUHUMI kikamilifu ili kuwa na utunzaji na utumiaji wa misitu ulio endelevu.

## 3.7 MAKAZI

### 3.7.3 Ukubwa wa eneo la makazi

Katika kijiji cha Muungano kuna makazi ya aina mbili; Makazi msongamano na makazi mashamba (makazi yaliyopo katika eneo la mashamba) hasa katika vitongoji vya Mnazi mmoja, Kipunga, Uleka, Naruwi na Likonde juu. Maeneo ya makazi msongamano yapo katika kitongoji cha Umoja na Ujamaa. Katika kijiji cha Muungano makazi yana ukubwa wa ha 4201.58

### 3.7.4 Mfumo na aina ya nyumba.

Katika kijiji cha Muungano aina za nyumba ni kama zifuatazo: nyumba za miti zilizokandikwa udongo na kuezekwa kwa nyasi/makuti, nyumba zilizojengwa kwa matofali ya udongo na kuezekwa kwa nyasi/makuti, nyumba zilizojengwa kwa matofali ya udongo na kuezekwa kwa bati na nyumba zilizojengwa kwa tofali za saruji na kuezekwa kwa bati. Hata hivyo Halmashauri ya kijiji cha Muungano haikuwa na takwimu za nyumba hizi. Kwa upande wa upatikanaji wa viwanja; Halmashauri ya kijiji cha Muungano husimamia ugawaji wa viwanja kwa wananchi wake hivyo huraisisha upatikanaji wa viwanja hivyo.

Katika kijiji cha Muungano nyumba nyingi ni za udongo zilizoezekwa kwa nyasi na nyingi hazikusakafiwa na hazina madirisha ya kupitishia hewa ya kutosha, Wanakijiji walio wengi hawana kipato cha kutosha cha kuwawezesha kujenga.


### 3.7.5 Vifaa vinavyotumika katika ujenzi na upatikanaji wake.

Ni pamoja na miti ya kujengea na kupaulia, nyasi za kuezekea, udongo wa kukandikia/kufyatulia matofali na kujengea, mbao kwa ajili ya kupaulia, kutengenezea milango, madirisha na mabati ya kuezekea. Vifaa vya ujenzi kama saruji, mabati na nondo vinapatikana mjini Lindi au Mnazimmoja. Vifaa hivi ni ghali, na kwa kuwa wanakijiji wengi wanakipato duni inapelekea wanakijiji hao kutumia vifaa vinavyopatikana kijijini kwa bei nafuu hivyo kufanya nyumba zao kuwa za kiwango cha chini ambazo wakati wa mvua zinavuja, kutokana na kuezekwa kwa nyasi na pia nyumba hazina mwanga wa kutosha kutokana na kutokuwa na madirisha au kuwa na madirisha madogo sana.

### 3.7.6 Shughuli nyingine ndani ya eneo la makazi.

Katika kijiji cha Muungano shughuli za biashara ndogo ndogo kama magenge, vioski, vilabu vya pombe, mashine za kusaga, maduka ya rejareja zinafanyika katika eneo la makazi ili kurahisisha upatikanaji wa mahitaji madogomadogo kwa wanakijiji. Hata hivyo kuna uwanja wa mpira na viwanja vingine vidogo vidogo vya michezo kwa ajili ya wanafunzi na watoto wadogo.

RAMANI YA KIJIJI CHA MUUNGANO MATUMIZI YA SASA YA ARDHI.




| Matumizi ya Eneo | Ukubwa wa Eneo_ha |
|---|---|
| Ghala Bovu | 0.04 |
| Klabu ya Pombe | 0.51 |
| Makazi Mashamba | 3622.75 |
| Makazi Msongamano | 578.83 |
| Mambo Elimu | 0.77 |
| Mashamba | 760.95 |
| Ofisi ya Kijiji | 0.02 |
| Uwanja wa unyago | 0.78 |
| Msitu wa Kijiji | 5514.99 |
| Jumla | 10479 |

## SURA YA NNE

### 4.0 MATATIZO YA MSINGI YA KIJIJI FURSA, VIKWAZO NA MIKAKATI

### 4.1 Matatizo ya kijiji cha Muungano.

Wakati wa kuandaa mpango huu wanakijiji walitanabaisha matatizo makuu yafuatayo:-

- Ukosefu wa Maji safi na salama – ***Ufumbuzi/;*** Kila kitongoji kupata Kisima Uibuaji wa miradi ufanywe kwa kila kitongoji.
- Hakuna shule ya Msingi
- Ukosefu wa Umeme
- Ukosefu wa zahanati
- Ukubwa wa kijiji unaleta matatizo katika utawala ukizingatia vitongoji vingine kuwa mbali na makao makuu ya kijiji.
- Ukosefu wa soko
- Barabara mbovu haipitiki mwaka mzima na hivyo kuwa na mawasiliano duni.
- Kukosa zana bora za kilimo na pembejeo kutokana na ukosefu wa mtaji kwa wakulima inayopelekea uzalishaji mdogo wa mazao
- Wanyama waharibifu wa mazao shambani na wanaowashambulia binaadamu.

### 4.2 FURSA ZILIZOPO

Fursa zilizopo na zinazoweza kusaidia katika kutatua matatizo yanayowakabili wanakijiji wa kijiji cha Muungano ni pamoja na uwepo wa ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo, wataalam wa kilimo na mifugo ingawa ni wachache. Nguvu kazi ipo ya kutosha hivyo kurahisisha uzalishaji wa mazao, wasimamizi wa maeneo hayo (Halmashauri ya kijiji ipo, Kamati ya ardhi ya kijiji nk), vyanzo vya maji, vifaa asilia vya ujenzi (Mchanga, mawe), Mradi wa MKUHUMI, sheria ndogo za kuhifadhi vyanzo vya maji, hata hivyo wanakijiji walitanabaisha kuwa fursa hizo zikitumika vizuri zinaweza kusaidia katika utatuzi wa matatizo haya.

### 4.3 VIKWAZO VILIVYOPO

Wanakijiji wa kijiji cha Muungano walitanabaisha kwamba ingawa fursa zipo kijijini lakini kuna vikwazo vinavyokwamisha utatuzi wa matatizo yanayowakabili wanakijiji hao. Vikwazo vilizotajwa ni pamoja na ukosefu wa wataalamu na Elimu, Vifaa vya ujenzi kutokuwapo kijijini (Bati, nondo nk), fedha kwa ajili ya gharama za ujenzi wa miundombinu.

Ukosefu wa mbegu bora na pembejeo kwa ajili ya kilimo cha kisasa, uharibifu wa mazingira hasa katika vyanzo vya maji na misitu, ukosefu wa elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na misitu, uhaba wa wataalamu wa wanyamapori, ukataji miti ovyo, uchomaji wa mkaa, kilimo cha kuhamahama, uchomaji moto misitu ovyo, kutokuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, kukosekana kwa sheria ndogo kijijini ambazo zingetumika kulinda rasilimali husika, kukosekana kwa elimu ya uhifadhi wa mazingira.

## 4.4 MIKAKATI YA KUTATUA MATATIZO YA KIJIJI

**Jedwali Na. 12: Changamoto, fursa, vikwazo na mikakati**

| Na. | Changamoto/matatizo | Fursa | Vikwazo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ukosefu wa Maji safi na salama | -Vyanzo vya maji vipo<br>-Mfuko wa maji upo<br>-Serikali ya kijiji<br>-Kamati ya maji<br>-Wahisani<br>-VLUM | -Ugumu wa kuchangia mfuko wa maji<br>-Uelewa mdogo kwa jamii kuhusu sera ya maji<br>-Gharama kubwa za ununuzi wa mashine za maji |
| 2. | Ukosefu wa shule ya Msingi walimu na nyumba za walimu | -Eneo la ujenzi<br>-Serikali ya kijiji ipo<br>-Nguvu kazi ipo<br>-Kamati ya shule ipo<br>-Eneo la ujenzi<br>-TASAF II ipo<br>-Baadhi ya vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kijijini | -Kukosa kujitolea<br>-Ukosefu wa fedha<br>-Uelewa mdogo wa wananchi juu ya sera ya Taifa ya uanzishaji wa shule za elimu ya msingi |
| 3. | Ukosefu wa Umeme | -Chanzo cha umeme wa jua<br>-Nguvu kazi ipo<br>-Serikali ya kijiji ipo<br>-Kamati ya ujenzi<br>-VLUM ipo<br>-Wahisani wapo | -Gharama kubwa za kuweka na uendeshaji<br>-Serikali haijawa na wazo la kutathmini mahitaji ya umeme.<br>-Kukosekana kwa elimu ya Matumizi ya Umeme wa jua. |
| 4. | Ukosefu wa Zahanati | -Eneo la ujenzi<br>-Nguvu kazi ipo<br>-Serikali ya kijiji ipo<br>-Kamati ya ujenzi<br>-VLUM ipo<br>-Wahisani wapo<br>-Baadhi ya vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kijijini | -Ukosefu wa fedha kwa ajili ya gharama za ujenzi<br>-Jamii kujitolea<br>-Uelewa mdogo wa jamii juu ya sera ya afya |
| 5. | Eneo kubwa kiutawala | -Serikali ya kijiji ipo<br>-Idadi ya watu inatosha kuwa na mgawanyiko<br>-VLUM ipo | -Kata kutopeleka maombi ya kijiji kwenda Halmashauri<br>-Gharama za kuanzisha kijiji |
| 6. | Ukosefu wa soko la kuuzia mazao | -Eneo la ujenzi<br>-Serikali ya kijiji ipo<br>-Kamati ya ujenzi<br>-VLUM ipo<br>-Mazao ya biashara yapo<br>-Nguvu kazi ipo<br>-Wahisani wapo | -Ukosefu wa fedha kwa ajili ya gharama za ujenzi |
| 7. | Ukosefu wa barabara | -Barabara ya zamani ipo<br>-Nguvu kazi ipo<br>-Kamati ya ujenzi ipo | -Ukosefu wa fedha<br>-Ukosefu wa mitambo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | -VLUM | |
| 8. | Ukosefu wa zana bora na pembejeo za kilimo | -Serikali ya kijiji ipo<br>-Afisa ugani yupo<br>-Kikundi cha mbegu kipo<br>-VLUM ipo | -Ukosefu wa fedha<br>-Bei kubwa ya ruzuku |
| 9. | Wanyama waharibifu wa mazao shambani na wanaowashambulia binaadamu | -Serikali ya Kijiji ipo<br>-Kamati ya Maliasili ipo<br>-VLUM ipo<br>-Idara ya wanyama pori Wilaya ya Lindi | -Elimu ya sera ya wanyamapori<br>-Uwezo mdogo wa jamii kufukuza wanyama waharibifu |

**Chanzo: Serikali ya Kijiji na kamati ya matumizi bora ya ardhi, 2011**

## 4.5 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI KWA USHIRIKISHWAJI JAMII

### 4.5.1 Mpango kazi wa jamii kijiji cha Muungano

**Jedwali Na. 13. Mpango kazi wa jamii kijiji cha Muungano.**

| No. | Lengo | Shughuli | Muda | Wahusika | | Mahitaji (nyenzo) | Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Ndani | Nje | | |
| 1. | -Kuwa na maji safi na salama | -Kutafuta chanzo cha maji chenye uhakika<br>-Kusafisha eneo la chanzo cha maji<br>-Kukusanya vifaa vya ujenzi, mawe na mchanga<br>-Kuanza kazi ya kuchimba | -Kuanzia Januari, 2011 | -S/Kijiji<br>-Wananchi<br>-VLUM<br>-Kamati ya maji | -H/Wilaya<br>-Idara ya Maji<br>-Wafadhili | -Mabomba, Pampu, Vifaa vya Ujenzi, Ulinzi, Oil, Usafiri, Posho ya ulinzi, Mafuta na Nondo | -Kuwa na maji safi na salama<br>-Kupunguza magonjwa ya milipuko<br>-Kupunguza mimba zisizo na wenyewe |
| 2. | -Kuwa na Shule ya Msingi | -Kusafisha eneo la ujenzi<br>-Kukusanya vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kijijini<br>-Usanifu wa jengo<br>-Kutafuta Mafundi<br>-Kuanza kazi | -Februari, 2011 | -Wanakijiji<br>-H/Kijiji<br>-Kamati ya kituo cha elimu<br>-VLUM | -H/Wilaya<br>-Idara ya Elimu<br>-MMEM<br>-Wahisani | -Vifaa vya Ujenzi<br>-Usafiri<br>-Posho<br>-Samani | -Kuwa na Shule ya Msingi kuondoa ujinga<br>-Kupunguza umbali wa kwenda shule |
| 3. | -Kuwa na Barabara inayopitika mwaka mzima | -Kusafisha eneo la barabara<br>-Kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, kokoto, mchanga na vifusi<br>-Usanifu wa barabara<br>-Kuchimba Mitaro na Ujenzi wa Makaravati | -Machi, 2011 | -S/kijiji<br>-H/Kijiji<br>-Wananchi<br>-VLUM | -H/Wilaya<br>-Idara ya Ujenzi<br>-Wahisani | -Vifaa vya Ujenzi wa Barabara<br>-Mitambo ya Ujenzi<br>-Fedha<br>-Wataalam wa Ujenzi | -Kuwa na Barabara itakayopitika mwaka mzima |
| 4. | -Kuwa na | -Kuandaa eneo la | -Mei, | -Wanakijiji | -H/Wilaya | -Vifaa vya Ujenzi | -Kuwa na |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Zahanati | ujenzi<br>-Kukusanya vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kijijini<br>-Usanifu wa jengo<br>-Kutafuta Mafundi<br>-Kuanza kazi | 2011 | -H/Kijiji<br>-VLUM<br>-Kamati ya kituo cha elimu | -Idara ya Afya<br>-Wahisani | -Usafiri<br>-Posho<br>-Samani | Zahanati/Mahali pa matibabu |
| **5.** | -Kugawa eneo la utawala | -Kukumbusha kugawa eneo la utawala ili kuwa na vijiji viwili<br>-Kuandaa mkutano wa kijiji<br>-Idadi ya watu (sensa)<br>-Muhtasari wa kikao kuwasilishwa kata ili kupelekwa wilayani | -Januari, 2011 | -S/Kijiji<br>-H/Kijiji<br>-VLUM<br>-Wananchi | -H/Wilaya<br>-Kamati ya Uchumi na Mipango<br>-Idara ya Ujenzi<br>-Wafadhili | -Shajala<br>-Fedha | -Kuwa na vijiji viwili kurahisisha utendaji wa kazi<br>-Urahisi wa kupatikana huduma za jamii |
| **6.** | -Kuwa na soko | -Kuandaa eneo la ujenzi<br>-Usanifu wa jengo<br>-Kukusanya wa vifaa<br>-Kutafuta Mafundi<br>-Kuanza kazi | -Juni, 2011 | -Wanakijiji<br>-H/Kijiji<br>-VLUM | -H/Wilaya<br>-Idara ya Ujenzi<br>-Wahisani | -Vifaa vya Ujenzi<br>-Usafiri<br>-Posho<br>-Samani | -Kuwa na Soko zuri la kuuzia bidhaa |
| **7.** | -Kuboresha zana za kilimo na pembejeo | -Kukopeshwa pembejeo za Kilimo kama dawa, mbegu bora na mbolea<br>-Ununuzi wa nyavu za kusakia wanyama waharibifu<br>-Ununuzi wa risasi za wanyama wakali | -Januari, 2011 | -H/kijiji<br>-S/Kijiji<br>-Wananchi<br>-VLUM<br>-Bwana shamba | -H/Wilaya<br>-Idara ya Kilimo<br>-Wahisani | -Mbegu bora, Madawa ya kuulia wadudu, Mbolea na Zana za kilimo<br>-Nyavu za kusakia wanyama<br>-Trekta | -Kuwa na Mavuno ya Kutosha<br>-Kupunguza njaa<br>-Kuondoa Umasikini kwa kuuza ziada ya Mazao |
| **8.** | -Kuzuia uchomaji moto hovyo wa Mazingira | -Kutoa elimu ya mazingira<br>-Kutunga sheria ndogo za kuzuia uharibifu wa mazingira | -Desemba, 2011 | -H/kijiji<br>-S/Kijiji/Wananchi<br>-Kati ya Maliasili<br>-VLUM | -H/Wilaya<br>-Idara ya Maliasili<br>-Wahisani<br>-Vikundi vya sanaa | -Vifaa vya Ujenzi<br>-Shajala<br>-Fedha<br>-Vitendea kazi | -Kuwa na mazingira mazuri<br>-Kuzuia mmomonyoko wa udondo<br>-Kutunza vyanzo vya maji |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na kamati ya matumizi bora ya ardhi, 2011.**

**SURA YA TANO**

# 5.0 MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI

## 5.1 UTANGULIZI

Kuna hatua kuu 6 katika utayarishaji mipango ya matumizi bora ya ardhi (PLUM, 1998), Hatua hizo ni:-

HATUA YA 1: Maandalizi ngazi ya wilaya – kuunda timu ya PLUM na kuipa Mafunzo

HATUA YA 2: PRA kijijini

HATUA YA 3: Upimaji zaidi – kuhakiki mipaka

HATUA YA 4: Utayarishaji rasimu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi

HATUA YA 5: Utarayarishaji na utekelezaji wa mipango ya kina ya ya kuendeleza maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali.

HATUA YA 6: Uimarishaji wa taasisi za kijiji ili ziweze kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji.

Kwa mujibu wa hatua hizo hapo juu, kazi ya utayarishaji mipango ya matumizi bora ya Ardhi ya kijiji cha Muungano imeishia hatua ya 4. Hata hivyo siyo kazi zote zilizotakiwa kufanyika ndani ya hatua 1 – 4 zimekamilika. Baadhi ya shughuli ambazo hazikukamilika ni pamoja na kufungua masjala ya ardhi, kupima mashamba na kuyasajili kwa kuanza kutoa hatimiliki za kimila.

## 5.2 MAHITAJI HALISI YA ARDHI KWA MATUMIZI MBALIMBALI

### 5.2.1 Utangulizi

Kwa jamii za wakulima wadogo na wachungaji waishio vijijini, shughuli zao huziendesha kwa ajili ya kujikimu kwanza na mambo ya ziada au utajirisho hufuata baadae; kimsingi hazipewi uzito mkubwa. Hali hii siyo tu imedumaza maendeleo yao bali pia imechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na hasa katika miaka michache iliyopita ambapo Tanzania haikuwa na sheria za Ardhi na matumizi yake. Aidha, hali hiyo ya kulima bila malengo na kukosekana sheria ya kukibana kilimo holela vile vile imechangia kushamili kwa tabia ya kilimo na uchungaji wa kuhamahama na hivyo kusasabisha uharibifu wa ardhi na rasilimali zake. Kimsingi kuna haja ya kuwepo malengo katika kuendesha kilimo na ufugaji.

Katika sura hii ya tano, jaribio linafanyika kuweka malengo ya mkulima na mfugaji kwa mtizamo wa uendeshaji shughuli zao kiuendelevu ili kuhakikisha mahitaji ya msingi ya jamii husika yanapatikana na wakati huo athari kwa ardhi na mazingira zinapunguzwa kwa viwango vinavyokubalika. Hii itawezekana baada ya kubainisha mahitaji halisi ya ardhi kwa matumizi mbalimbali kwa kuzingatia ukulima na ufugaji wa kisasa.

Mahitaji ya wakulima na wachungaji ni ya aina mbili, kwanza kuzalisha chakula chao na pili ni kupata fedha kutokana na mauzo ya mazao yao ili wapate fedha ya kununulia

bidhaa muhimu wasizoweza kuzalisha wao wenyewe hususani bidhaa za viwandani na huduma mbalimbali zinazolipiwa fedha taslimu mfano tiba, michango ya kijamii na ada za shule.

#### 5.2.1.1 Mahitaji ya mazao ya chakula

Mazao makuu ya chakula katika kijiji cha Muungano ni mahindi, mtama, mpunga na muhogo. Kitaalamu ukadiriaji wa mahitaji ya chakula katika kaya ni muhimu katika kuhakikisha familia hasa za vijijini zinakuwa na chakula cha kutosheleza mahitaji ya mwaka mzima. Kaya ikifahamu mahitaji yake itaweka mipango thabiti ya uzalishaji kulingana na mahitaji ya chakula na matumizi mengine.

Kwa watu wa Muungano idadi ya milo ni 2 mchana:- ni Ugali wa mahindi na Jioni ni wali/ugali. Mahitaji ya mahindi kwa kaya kwa mwaka ni magunia 5.5 ya mahindi sawa na ekari 1.8 za Mahindi kwa kaya. Eneo linalohitajika kwa wananchi wa kijiji cha Muungano kwa kaya moja baada ya kuangalia mazao yote ya chakula ni ekari 4. Kijiji kina kaya 650 hivyo eneo la ardhi kwa zao la chakula kwa mwaka ni ekari 2600 na baada ya miaka ishirini eneo la kilimo kwa chakula litakuwa ekari 3084.

#### 5.2.1.2 Mahitaji ya zao la biashara

Zao kuu la biashara ni ufuta na pato tarajiwa ili kukidhi mahitaji muhimu ya kaya kwa mwaka ni Tshs 904,680/= ambapo zinahitajika jumla ya kilo 905 sawa na gunia 9 za ufuta ambazo zitazalishwa kutoka kwenye shamba la Ukubwa wa eka 3. Kwa hivyo mahitaji ya eneo la ardhi kwa zao la biashara litakuwa ekari 1950 zinazotakiwa zilimwe kwa kaya zote kwa mwaka ili kukidhi mahitaji na baada ya miaka ishirini mahitaji yatakuwa ekari 2313.

### 5.2.2 Mahitaji ya kuni

Kwa wastani mtu 1 anahitaji 1.5 $m^3$ kwa mwaka, na idadi ya watu wote kijijini ni 2471 na mahitaji ya nishati kwa mwaka kwa watu wote ni mita za ujazo 3707. Msitu una uwezo wa kutoa ujazo wa kuni mita za ujazo 1.8 kwa ekari. Hivyo mahitaji ya eneo la ardhi kwa nishati kwa mwaka kwa kaya zote ni ekari 2059 na baada ya miaka 20 mahitaji yatakuwa ekari 2569.

### 5.2.3 Mahitaji ya ardhi kwa ajili ya mifugo

Kijiji cha Muungano mwaka 2011 kina idadi ya mifugo ambayo ni mbuzi 321, bata 9 na kuku ni 2600. Uwiano wa kitaalamu wa kipimo cha mifugo (Livestock Unit) ni kama ilivyowekwa kwenye jedwali Na. 11.

### 5.2.4 Mahitaji ya maji kwa ajili ya binadamu.

Kwa wastani binadamu anahitaji lita 20 - 30 za maji kwa siku kwa matumizi ya nyumbani, ambayo ni pamoja na kunywa, kupika, kufulia n.k. Hivyo hivi sasa mahitaji ya maji kwa siku kwa matumizi ya nyumbani (idadi ya watu 2471) ni lita 49420 mpaka lita (74,130), mahitaji ya maji kwa matumizi ya nyumbani kwa wanakijiji wote baada ya mwaka mmoja yatakuwa hadi lita 27,057,450.

### 5.2.5 Mahitaji ya maji kwa ajili ya mifugo

Kwa wastani kipimo kimoja cha mfugo (livestock unit) hutumia maji kulingana na uzito wake kwa maji ya kunywa. Ng'ombe inaweza kutumia hadi lita 25 - 30 kwa siku. Mifugo iliyopo katika kijiji cha Muungano ni Mbuzi ambao wapo 321 na kwa mbuzi mmoja anatumia maji lita 2 – 3 kwa siku. Hivyo, hivi sasa mahitaji ya maji kwa mifugo (L.U 321) ni lita 642 mpaka 963 kwa siku. Baada ya mwaka mmoja mahitaji ya maji kwa (L.U 321) yatakuwa lita 234330 mpaka lita 351,495.

### 5.2.6 Huduma za kijamii

Viwango vifuatavyo vya eneo la ardhi inashauriwa vitolewe kwa kila aina ya matumizi yanayohusu huduma za jamii. Viwango hivyo vimependekezwa kwenye mwongozo wa PLUM (1998)

| MATUMIZI | VIWANGO | ENEO (ha) |
|---|---|---|
| Zahanati | 5000m2 (0.5ha) | 0.5 ha |
| Shule ya Msingi (wanafunzi) 280-1120) | 1.2-4.5ha(zipo2) | 9.0 ha |
| Shule ya Sekondari | 2.5 – 5.0 ha | 5.0 ha |
| Kiwanja cha michezo | 10 ha | 10.0 ha |
| Soko | 0.5 – 1.5 ha | 1.0 ha |
| Maduka | 1.0 – 2.0 ha | 2.0 ha |
| Majengo ya umma | 0.32 – 1.5 ha | 1.5 ha |
| Biashara na huduma | 0.16 – 0.5 ha | 0.5 ha |
| Maeneo ya dini | 0.2 – 0.4 ha (kila dini) | 2.0 ha |
| Makaburi | 2.0 ha (kila kitongoji) | 4.0 ha |
| | **Jumla** | **35.5 ha** |

Kwa sasa kati ya huduma zilizotajwa hapo juu kuna ambazo tayari zipo na zingine hazipo lakini inatarajiwa ifikapo mwaka 2031 huduma zote zitakuwapo kama zilivyoorodheshwa hapo kijijini.

## 5.3. MAPENDEKEZO

### 5.3.1. Mgawanyo wa ardhi

Kutokana na mikutano ya ushirikishwaji jamii iliyofanywa na timu ya PLUM katika kijiji cha Muungano wanakijiji walipendekeza matumizi ya ardhi kama ilivyoonyeshwa kwenye jendwali.


**Jedwali Na.14: Mapendekezo ya mpango wa matumizi ya ardhi.**

| Na. | Aina ya matumizi | Mipaka ya eneo | Ukubwa wa eneo (ha) |
|---|---|---|---|
| 1. | Eneo la kilimo | Maeneo ya kilimo kwenye vitongoji vya Umoja na Ujamaa ni kuanzia Namngumi, mpaka Mtonya kaskazini mwa kijiji cha Muungano, kwa Mnazi mmoja litakuwa Michee mpaka Livoche kusini magharibi mwa kijiji. Kitongoji cha Uleka litakuwa Mpeye kaskazini mwa kitongoji na eneo jingine ni kwa Mandani kusini magharibi mwa Kitongoji. Kitongoji cha Likonde juu eneo litakuwa ni kilimo makazi. Naruwi litakuwa ni Chinyung'unya mpakani na Michee. Kitongoji cha Kipunga nimependekezwa Namkunula, Kiwambala, Kimbuto na Mmale magharibi mwa Kijiji cha Muungano | 623.81 |
| 2. | Eneo la makazi | Eneo la Makazi kijiji cha Muungano limependekezwa kuwa litaanzia kwa Binti Mturo kusini mwa kijijimpaka kwenye pacha ya kuelekea Naruwi kwa Maanje kuegemana na Mlima Namwanda, kwa Rashidi Namayanomagharibi mwa kijiji. | 5237.58 |
| 3. | Eneo la huduma za jamii | Eneo la huduma za jamii limependekezwa kwa bwana Juma Msiniuzi mpaka milima ya Ugulya kusini mwa kijiji cha Muungano | |
| 4. | Hifadhi ya vyanzo vya maji | Maeneo ya vyanzo vya maji yamependekezwa kuwa ni Chinyova, kwa hafai, kwa mtamile, kwa mtawa , Mmale, kwa Nakulyoni, kwa Pakia, kwa Namanyai, Kwa Mkunje, Kwa Namayano, Likandilo, Mtonya Mpeye, Namkunula, Kipunga, Mivombwe, Namwirondo, Kwa Mng'apuka na Kwa Manga. | |
| 5. | Misitu ya hifadhi | Katika kutenga eneo hili, mwanzo ulitengwa pia msitu kwa ajili ya uvunaji wa rasilimali mbalimbali zinazohitajika na jamii kwa maisha ya kila siku kama vile majengo, mbao, fito, kuni nk; lakini imekubalika kuwa rasilimali hizi zitachukuliwa pia hata kwenye msitu wa hifadhi, hivyo hakuna haja ya kuyatenganisha maeneo haya. Msitu wa hifadhi wa kijiji cha Muungano umezunguka kutoka Likandilo, Mkaleka, makuani, Michee, Namwilondo, Naluwi, kwa | 4614.17 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Jumanne, Kiwambala, Kipunga, makewe, Mpelenganya, Kikonde mwana (Noto) na kupakana na vijiji vya Mkombamosi Kinyope na Milola magharibi. Misitu mingine ambayo kwa pamoja ndiyo inayounda msitu wa hifadhi wa kijiji cha Muungano ni Machaninga, Makuani na Likonde juu. | |
| 6. | Eneo la malisho | Eneo hili limependekezwa kuwa katika eneo la Likandilo ya Mkaleka katika kitongoji cha Mnazi mmoja kusini mwa kijiji cha Muungano. | |
| 7. | Eneo la makaburi | Vitongoji vya ujamaa, Umoja na Mnazi mmoja, eneo la makaburi litakuwa ni kwa Makolela.<br><br>Kitongoji cha Kipunga eneo la makaburi litakuwa ni Namamndenge kwa mnyou na kwa kipando<br><br>Naruwi – Kwa Mkopa<br><br>Uleka kwa Mtoyomba, kwa Abedi, kwa Nampanya na kwa Mtemeka.<br><br>Likonde juu – Kwa Makwaila | |

**Chanzo: Serikali ya kijiji na kamati ya matumizi bora ya ardhi, 2011**

RAMANI YA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI




## Ramani ya Kijiji cha Muungano kuonyesha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi 2011-2031

Projection: WGS 84 UTM Zone 37 S
Map Dutum: WGS 84

Ramani hii ni kwa ajili ya kusaidia vijiji kupanga matumizi bora ya ardhi. Imeandaliwa na wanakijiji wakishirikiana na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kupitia mradi wa MKUHUMI (REDD).

| Matumizi ya Eneo | Ukubwa wa Eneo_ha |
|---|---|
| Ghala bovu | 0.04 |
| Huduma za jamii | 0.00 |
| Kilabu cha Pombe | 0.51 |
| Makaburi | 1.23 |
| Makazi Mashamba | 4660.64 |
| Makazi Msongamano | 576.95 |
| Mambo Elimu | 0.77 |
| Mashamba | 623.81 |
| Msitu wa Hifadhi wa Kijiji | 4614.17 |
| Uwanja wa Unyago | 0.78 |
| Tambiko Nangumi | 0.01 |
| Jumla | 10479 |

| | | TAREHE/SAHIHI |
|---|---|---|
| IMEKAGULIWA NA | MKURUGENZI MKUU TUME TA TAIFA NA MATUMIZI BORA YA ARDHI | |
| IMEPITISHWA NA | MKUTANO MKUU WA KIJIJI CHA MUUNGANO | |
| IMERIDHIWA NA | HALMASHAURI YA WILAYA | |
| | KAMATI YA UCHUMI NA UJENZI NA MAZINGIRA(W) | |
| IMETANGAZWA NA | WAZIRI | |
| IMETAYARISHWA NA | HALMASHAURI YA KIJIJI | |

### Kielelezo

- Barabara
- Ghala bovu
- Huduma za jamii
- Kilabu cha Pombe
- Makaburi
- Makazi Mashamba
- Makazi Msongamano
- Mambo Elimu
- Mashamba
- Msitu wa Hifadhi wa Kijiji
- Tambiko Nangumi
- Uwanja wa Unyago

### 5.3.2 Upimaji wa maeneo

Baada ya mapendekezo ya mgawanyo wa Ardhi ya kijiji kwa matumizi makuu (kilimo, makazi, hifadhi, malisho, huduma za jamii) kukubaliwa na kuidhinishwa na mkutano wa kijiji, shughuli inayofuata ni kuyapima maeneo hayo na kuyaingiza kwenye ramani ya kijiji kwa ajili ya kumbukumbu. Upimaji hufanyika kwa kutumia GPS (handheld GPS) lakini kabla ya kifaa hiki hakijatumika lazima kirekebishwe vipimo na kuwekwa katika mizania *calibration*) ili kupunguza uwezekano wa kupata vipimo visivyosahihi. Mpima pamoja na timu ya VLUM na wanakijiji watazungukia kila eneo lililotengwa na kuhakikisha vipimo vya kutosha kuingiza eneo hilo kwenye ramani vimechukuliwa na kila eneo panapochukuliwa kipimo alama ya kudumu (katani, minyaa, miti ya kuchipuka) inapandwa eneo hilo kwa ajili ya kumbukumbu ya wanakijiji husika.

Baada ya zoezi la hapo juu, inafuata kazi ya kuhakiki ukubwa wa maeneo hayo; hii inafanyika kwenye ramani. Mpima atahakikisha ukubwa wa maeneo yaliyopimwa unalingana na mapendekezo yaliyokubaliwa na wahusika.

Kimsingi kazi ya kupima maeneo na kuyaingiza kwenye ramani baada ya kupitishwa na mkutano wa kijiji ni hitimisho la awamu ya kwanza ya utayarishaji mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hadi hatua hii kijiji kinakuwa na rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji. Ili mpango huu uweze kumpa mkulima faida tarajiwa ni lazima kuanzisha mchakato wa awamu ya pili ambayo inahusu utayarishaji wa mipango shirikishi ya kina ya kuendeleza maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali ili kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji cha Muungano.

### 5.3.3 Mpango wa kuendeleza maeneo yaliyotengwa.

Mipango ya matumizi bora ya ardhi haiishii kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi makuu mbalimbali, mfano, kilimo, makazi, malisho ya mifugo, vyanzo vya maji, huduma za jamii n.k. utengaji maeneo peke yake hauongezi uzalishaji kwa namna yeyote ile, lazima zoezi hilo lifuatishwe na utayarishwaji mipango shirikishi ya kina ya kuendeleza maeneo yaliyotengwa (detailed management plans) kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Kwa hiyo kila aina ya matumizi yaliyotengewa ardhi lazima yatayarishiwe mipango ya namna gani yatumike ili kuleta faida kubwa na endelevu. Kazi hii inatarajiwa ifanywe na Halmashauri ya wilaya (mwenye dhamana hiyo) kupitia idara zake, mfano Idara ya kilimo itayarishe mpango shirikishi wa kuendeleza eneo la mashamba, Idara ya maliasili na mradi wa MKUHUMI zitayarishe mpango wa kuendeleza eneo la msitu wa Hifadhi, Ardhi ishughulikie eneo la makazi n.k.

Ni kupitia utekelezaji mipango ya kina ya kuendeleza maeneo, kama ilivyosemwa awali, uzalishaji unaweza kuongezeka na hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji kutaleta matokeo tarajiwa ambayo ni mkulima kuwa na maisha bora. Suala la mpango gani wa kuendeleza maeneo utayarishwe mwanzo litategemea na vyanzo vya fedha za kugharimia kazi hiyo na utashi wa jumuiya ya kijiji husika. Lakini katika hali ya kawaida suala la eneo la kilimo na eneo la Msitu wa Hifadhi wa kijiji cha Muungano kupitia mradi wa MKUHUMI yanastahili kutayarishiwa mipango ya kina kwanza.

### 5.3.4 Kazi zitakazofuata.

Kazi zitakazofuata ni pamoja na;

- Kujenga na kufungua masjala ya ardhi ya kijiji
- Serikali ya kijiji mara baada ya kukamilisha ujenzi wa masjala ya kijiji itawasiliana na bwana ardhi wa wilaya ili kupanga uzinduzi wa masjala hiyo.
- Kuanza kazi ya upimaji maeneo ya umma na binafsi na kuyasajili
- Mafunzo kwa uongozi wa kijiji jinsi ya kusimamia ardhi (utawala wa ardhi)
- Mafunzo ya kina kwa uongozi jinsi ya kusimamia daftari la ardhi la kijiji
- Kutoa mafunzo kwa baraza la ardhi la kijiji
- Kazi zote zilizobakia kukamilisha hatua 1 – 4 za PLUM
- Kuwasilisha mpango na sheria ndogo wilayani na wizarani ili upitishwe. Hii ni jukumu la serikali ya kijiji, VLUM na Bwana Ardhi wa wilaya.

**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MUUNGANO WILAYA YA LINDI**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**NAMBA 7 YA MWAKA 1982)**

**SHERIA NDOGO YA KIJIJI ( VILLAGE BY-LAW)**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 168*

## SHERIA NDOGO ZA USIMAMIZI WA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI ZA KIJIJI

*Jina* **1.** Sheria Ndogo hizi ziitwe "SHERIA YA USIMAMIZI WA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARDHI YA KIJIJI CHA MUUNGANO WILAYA YA LINDI, YA MWAKA 2012" na zitaanza kutumika mara zitakapoidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya ya LINDI.

*Matumizi* **2.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo ya Kijiji cha Muungano kwa ajili ya kuratibu shughuli za mpango wa matumizi bora ya ardhi. Matumizi ya Sheria Ndogo hizi yatakuwa mara baada ya kupitishwa katika ngazi ya Kijiji na wilaya

*Tafsiri ya maneno* **3.** **''Eneo la Kilimo (mashamba)'':** Maana yake ni eneo la uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

**''Eneo la makazi mashamba'' :** Maana yake ni eneo lenye makazi mtawanyiko na linatumika kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara

**''Eneo la malisho'':** Maana yake ni pori la miti na nyasi linaloweza kutumika kama malisho na/au manywesheo ya mifugo.

**"Halmashauri ya Kijiji"** Maana yake ni Halmashauri ya Kijiji cha Muungano, iliyoundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa ( Tawala za wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982

**''Huduma za jamii''** Maana yake ni huduma za kijamii kama vile elimu, afya, barabara, ibada na taasisi nyinginezo ndani ya eneo la makazi ya pamoja.

''**Kamati ya Maliasili**" Maana yake ni Kamati iliyoundwa na wanaKijiji na kuidhinshwa na mkutano wa Kijiji ili kuisaidia kazi za usimamizi wa misitu yote iliyopo ndani ya Kijiji husika ikiwemo misitu ya hifadhi.

**"Kamati ya Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji"** Maana yake ni kamati iliyoundwa na Halmashauri ya Kijiji na kuidhinishwa na mkutano wa

Kijiji ili kuisaidia kazi za usimamizi wa matumizi ya ardhi ya Kijiji.

**''Makazi''** Maana yake ni maeneo yanayokaliwa na watu kwa kujengwa nyumba za kuishi au biashara. Maeneo haya yana ukubwa wa robo ekari kwa kila kaya.

"**Mgeni**" Maana yake ni mtu asiye mkazi wa Kijiji cha Muungano, awe Mtanzania au sio Mtanzania

"**Mifugo**" Maana yake ni wanyama wote wafugwao ambao huishi kwa kula miti na nyasi, hii ni kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda n.k

**"Mkutano wa Kijiji"**Maana yake ni Mkutano wa wanakijiji wa Muungano unaoitishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ( Tawala za wilaya ) Na. 7 ya mwaka 1982.

**"Msitu**"Maana yake ni mkusanyiko wa nyasi, vichaka vinene, miti ya asili na miti ya kupandwa kwa matumizi mbalimbali.

**''Msitu wa Hifadhi**" Maana yake ni msitu uliotengwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu

**"Serikali"**Maana yake ni Serikali ya Kijiji cha Muungano **"**

**''Vyanzo vya Maji'':** Maana yake ni chemichemi, mito, visima, mabwawa, na mabonde yenye maji.

*Mahusiano ya Mkutano wa Kijiji, Halmashauri ya Kijiji na Kamati mbalimbali*

**4.** Sheria mama ya nchi , inatoa mamlaka kwa Halmashauri ya Kijiji kuteua na kuunda Kamati kuisaidia kutekeleza majukumu yake, kadri inavyoona inafaa. Katika kufanya kazi zake, Kamati sharti iwajibike, itoe taarifa na kupata idhini ya Halmashauri ya Kijiji. Kwa mintarafu hii, Kamati inawajibika kwa Halmashauri ya Kijiji, na Halmashauri ya Kijiji inawajibika kwa Mkutano wa Kijiji. Mawasiliano na mtu au taasisi nje ya Kijiji ni baina na Halmashauri ya Kijiji.

*Kutenga na kuonyesha maeneo ya matumizi yaliyotengwa*

**5.** Maeneo ya matumizi yaliyopangwa yametengwa na kuonyeshwa kwa ramani, iliyoambatishwa katika Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji. Katika ardhi (uwandani) vitawekwa vibao vinavyoonyesha mwanzo na mwisho wa matumizi ya ardhi yaliyoidhinishwa. Halmashauri ya Kijiji itahakikisha vibao hivi vinakuwepo siku zote. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuondoa au kuharibu kwa njia yoyote ile vibao hivi.

*Usimamizi na uendelezaji*

**6.** Usimamizi na uendelezaji wa maeneo yaliyopangwa utakuwa kama ifuatavyo:-

**(i) Eneo la Makazi**

*wa maeneo yaliyotengwa*

Ujenzi katika eneo la makazi ni sharti ufuate kanuni za afya bora ikiwemo kuzingatia nyumba bora za kudumu, na kila nyumba kuwa na choo. Eneo la makazi litaendelea kupanukia katika eneo la kilimo (mashamba) kwa utaratibu wa mhitaji kukubaliana na kununua toka kwa mmiliki wa shamba. Wamiliki wahimizwe kusajili maeneo ya makazi yao na kupata hatimiliki za kimila kwa maeneo yaliyochini ya serikali ya Kijiji; wakati eneo la kimipango miji litatolewa hati za kiserikali. Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji (VLUM) na Kamati ya Afya vitasimamia uendelezaji wa maeneo haya kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji na Halmashauri ya wilaya ya Lindi Vijijini kupitia idara husika.

**(ii) Eneo la Kilimo (Mashamba)**

Uendelezaji uzingatie kanuni za kilimo bora endelevu na hifadhi ya ardhi na maji. Halmashauri ya Kijiji ihakikishe mashamba darasa ya mazao mbalimbali yanakuwepo katika kila kitongoji, ambapo wanaKijiji watajifunzia na kufuata katika mashamba yao ili kuongeza uzalishaji kwa kila ekari. Wamiliki wahimizwe kusajili mashamba yao na kupata hatimiliki za kimila. Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji (VLUMC), itasimamia uendelezaji wa eneo hili kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji.

**(iii) Eneo la Huduma za Jamii**

Huduma nyingi za jamii zitatengewa maeneo katika eneo lililoainishwa kadri zinavyohitajika. Wakati bado sehemu za eneo hili hazijaendelezwa,ni marufuku kwa watu binafsi kupanda mazao ya kudumu au kujenga nyumba katika eneo hili. Aidha wakati eneo hili linaendelezwa, hapatakuwa na fidia kwa mtu yeyote, bali Halmashauri ya Kijiji inaweza kuwapa fursa wenye mazao ya muda kuvuna mazao yao. Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji (VLUMC), itasimamia uendelezaji wa eneo hili kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji.

**(iv) Misitu ya Hifadhi ya Kijiji**

Maeneo yaliyoainishwa yapimwe, yasajiliwe, kuendelezwa na kuhifadhiwa kama misitu ya hifadhi ya Kijiji. Ni marufuku kufyeka, kuchoma moto, na kuchungia katika maeneo haya. Uvunaji wa mazao ya misitu ni lazima upate kibali cha maandishi cha Halmashauri ya Kijiji. Kamati ya Maliasili na Mazingira itasimamia maeneo haya kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji.

**(v) Maeno ya Hifadhi ya Vyanzo vya Maji**

Maeneo ya vyanzo vya maji yaliyoainishwa yapimwe, yasajiliwe, kuendelezwa na kuhifadhiwa kama vyanzo vya maji. Ni marufuku kufyeka, kuchoma moto, kuchoma mkaa, kulima na kuchungia katika maeneo haya bila ya kibali cha maandishi cha Halmashauri ya Kijiji. Kamati ya Maji itasimamia maeneo haya kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji.

**(vi) Eneo la nyanda za Malisho ya Mifugo**

Maeneo ya malisho ya mifugo yaliyoainishwa yapimwe, yasajiliwe, na kuendelezwa kama nyanda za malisho na manywesheo. Ni marufuku kufyeka, kuchoma moto, kuchoma mkaa, na kulima katika haya. Wafugaji watajenga nyumba za makazi na mazizi ya mifugo katika maeneo ya mashamba kandokando ya eneo hili kwa utaratibu utaratibu utakaotolewa na Halmashauri ya Kijiji kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam wa Idara ya mifugo ya wilaya itaainisha idadi ya mifugo inayopaswa kuwemo katika eneo hili. Mifugo ya ziada ni sharti ivunwe kwa kuuzwa kwa maendeleo ya wafugaji na Kijiji kwa ujumla. Wafugaji waunde kamati itakayosimamia ufugaji endelevu, na kuweka wakati wote kumbukumbu ya idadi ya mifugo kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji. Ni marufuku kuchungia au kunyweshea mifugo nje ya eneo lililotengwa kwa shughuli ya ufugaji. Vilevile ni marufuku kuchoma moto samadi inayotokana na mifugo bali itumike kwa kilimo kurutubisha ardhi ya Kijiji. Hadi hapo itakapoundwa Kamati ya Wafugaji, Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji itasimamia eneo hili kwa niaba ya Halmashauri ya Kijiji.

*Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi*

**7.** Mabadiliko ya matumizi ya ardhi katika eneo lolote lililoainishwa yatafanyika tu kwa Halmashauri ya Kijiji kurejea (review) na kurekebisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji na kupata ridhaa ya Mkutano wa Kijiji.

*Adhabu*

**8.** Mtu yeyote anayethibitika kutenda kosa na kukiuka Sheria hizi; atashitakiwa kwa mujibu wa Sheria mama ya Nchi na akipatikana na hatia atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs. 50,000/= na kuamriwa kurekebisha/kurejesha katika hali ya awali eneo lililoharibiwa au kulipa fidia ya uharibifu uliofanyika. Mchanganuo wa makosa na adhabu zake katika matumizi mbalimbali ya Ardhi

*Eneo la kilimo*

**9.** **a)** Ni marufuku kulisha mifugo katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo. Atakayebainika kulisha mifugo katika eneo lililotengwa kwa

ajili ya kilimo mnyama wake atakamatwa na muhusika kuwajibika kulipa faini ya Tshs. 5,000/= na kulipia fidia mazao alioharibu.

b) Ni marufuku kuanzisha moto katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo. Atakayebainika kuwasha moto eneo la kilimo atatozwa faini isiyozidi Tshs. 50,000/= au kushitakiwa kwa mujibu wa Sheria mama ya Nchi

c) Ni marufuku kujenga kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo. Atakayebainika kujenga nyumba katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kilimo, Serikali ya Kijiji itamwita na kumuonya. Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa nyumba hiyo na muhusika kulipia gharama za ubomoaji.

d) Ni marufuku kuacha shambapori kwa muda wa miaka mitatu mfululizo, atakayebainika kuacha shamba pori kwa muda wa miaka 3 mfululizo serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kufanyia usafi, akikahidi serikali ya Kijiji itamnyang'anya na kumpatia mtu mwingine kuweza kulifanyia usafi.

*Eneo la makazi*

**10.** a) Nyumba katika eneo la makazi zitajengwa kwa kufuata kanuni za afya bora. Nyumba zitajengwa kwa kufuata mitaa na kila nyumba ni sharti iwe na choo.

b) Atakaejenga nyumba bila choo Serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kujenga choo. Akikaidi atalazimika kulipa faini ya Tsh 10,000/=na kujenga choo kwa lazima.

c) Ni marufuku kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi, atakayebainika kulima katika eneo la makazi Serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kung`oa mazao yake. Akikaidi Serikali ya Kijiji itang`oa na muhusika atalazimika kulipia gharama za ung`oaji.

d) Katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi inaruhusiwa kupanda miti ya matunda kama michungwa, Mipapai na Mipera. Ni marufuku kupanda minazi katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi.Atakaebainika kupanda minazi katika eneo la makazi Serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kung`oa. Akikaidi Serikali ya Kijiji itang`oa na muhusika kulipia gharama za ung`oaji.

e) Ni marufuku kuanzisha moto katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi. Atakayebainika kuanzisha moto katika eneo la makazi atatozwa faini isiyozidi Tshs. 50,000/=

f) Ni marufuku kuacha kiwanja pori katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makazi. Atakayebainika kuacha kiwanja pori kwa muda zaidi ya miaka 1, Serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kufanya usafi.

Akikaidi Serikali ya Kijiji itamnyang`anya na kumpatia mtu mwingine atakaeweza kufanyia usafi.

g) Ni jukumu la kila mkazi kufanya usafi katika barabara za mitaa zinazopita katika nyumba yake. Atakaebainika kutofanya usafi katika barabara za mitaa zinazopita katika eneo lake Serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kufanyia usafi. Akikaidi atatozwa faini ya Tsh 5,000/= na kulazimika kufanya usafi.

*Eneo la huduma za jamii*

**11.** a) Ni marufuku kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya huduma za jamii. Atakaebainika kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya huduma za jamii Serikali ya Kijiji itamwita na kumueleza kung`oa mazao yake, Akikaidi Serikali ya Kijiji itang`oa na muhusika atalazimika kulipia gharama za ung`oaji.

b) Ni marufuku kujenga katika eneo lililotengwa kwa ajili ya huduma za jamii, atakayebainika kujenga nyumba katika eneo la huduma za jamii, serikali ya Kijiji itamwita na kumuelekeza kubomoa nyumba yake, Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa na muhusika kulipia gharama za ubomoaji.

c) Ni marufuku kulisha mifugo katika eneo la huduma za jamii, Atakaebainika kulisha mifugo katika eneo hili atatozwa faini ya Tsh. 5,000/= kwa kila mnyama na kulipa gharama za uharibifu uliofanywa na mifugo yake.

d) Ni marufuku kuanzisha moto katika eneo lililotengwa kwa ajili ya huduma za jamii, atakaeanzisha moto atatozwa faini ya Tsh 50,000 .

*Eneo la vyanzo vya maji*

**12.** a) Ni marufuku kulima au kujenga katika eneo lililotengwa kwa ajili ya chanzo cha maji. Atakaebainika kulima au kujenga katika eneo lililotengwa kwa ajili ya chanzo cha maji atalazimika kubomoa nyumba yake au kung`oa mazao yake. Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa nyumba au kung`oa mazao yake na muhusika kulipia gharama za ubomoaji.

b) Ni marufuku kufanya shughuli zozote za kibinadamu kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya chanzo cha maji kwa umbali wa mita 200. Shughuli za kibinadamu ni pamoja na kufua, kuoga, kuosha vyombo na kulima, Atakaebainika kufanya shughuli za kibinadamu kwenye chanzo cha maji atatozwa faini ya Tsh.50, 000/=

c) Ni marufuku kuanzisha moto kwenye chanzo cha maji, Atakaebainika kuanzisha moto kwenye chanzo cha maji atatozwa faini ya Tsh. 50,000/=

*Eneo kwa ajili ya*

**13.** a) Maeneo ya pori na malisho ya mifugo yaliyoainishwa yapimwe, yasajiliwe, na kuendelezwa kama pori, malisho na manywesheo ya

*Malisho* mifugo. Hivyo eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho litumike kwa dhumuni hilo tu.

b) Hairuhusiwi kulima, kufyeka, kuchoma moto au kujenga katika eneo hilo. Atakayekiuka utaratibu huu atatozwa faini ya Tsh. 50,000/= au kuhukumiwa kwa mujibu wa Sheria mama ya Nchi

*Eneo kwa ajili ya msitu wa hifadhi*

**14. a)** Ni marufuku kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya msitu wa hifadhi. Atakayebainika kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya msitu wa hifadhi Serikali ya Kijiji itamwita na kumueleza kubomoa au kung`oa mazao yake. Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa au kung`oa mazao na muhusika kulazimika kulipia gharama za ubomoaji au ung`oaji.

**b)** Uvunaji katika misitu ya hifadhi ya Kijiji cha Muungano ni kulingana na sheria ndogo za usimamizi shirikishi wa misitu katika Kijiji cha Muungano. Atakaebainika kukiuka utaratibu huu atatozwa faini Tsh. 50,000 na mali alizovuna pamoja na vifaa alivyotumia kuvunia kutaifishwa na Serikali ya Kijiji.

**c)** Ni marufuku kuanzisha moto katika eneo lililotengwa kama Msitu wa hifadhi. Atakaebainika kuanzisha moto katika Msitu wa hifadhi atalipa faini ya Tshs 50,000/= au kushitakiwa kwa mujibu wa Sheria mama ya Nchi

**d)** Ni marufuku kulisha mifugo katika eneo lililotengwa kwa ajili ya msitu wa hifadhi. Atakayebainika kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya msitu wa hifadhi atatozwa faini ya Tsh 5,000/= kwa kila mmyama.

*Eneo la matambiko*

**15.** a) Ni marufuku kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya matambiko. Atayebainika kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya msitu wa hifadhi Serikali ya Kijiji itamwita na kumueleza kubomoa au kung`oa mazao yake. Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa au kung`oa mazao na muhusika kulazimika kulipia gharama za ubomoaji au ung`oaji.

*Eneo la makaburi*

**16.** a) Ni marufuku kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makaburi. Atayebainika kujenga au kulima katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makaburi, Serikali ya Kijiji itamwita na kumueleza kubomoa au kung`oa mazao yake. Akikaidi Serikali ya Kijiji itabomoa au kung`oa mazao na muhusika kulazimika kulipia gharama za ubomoaji au ung`oaji.

b) Ni marufuku kuanzisha moto katika eneo lililotengwa kwa ajili ya makaburi. Atakayebainika kuanzisha moto katika makaburi atalipa faini ya Tshs 50,000/=

*Kupitishwa na kusainiwa*

**17.** Sheria Ndogo hizi zimetungwa na Halmashauri ya Kijiji cha Muungano tarehe 05/08/2011 na kuidhinishwa na mkutano wa Kijiji cha Muungano tarehe 22/08/2011

Zimesainiwa:

Sahihi ............

Jina RASHIDI S. RASHIDI

**AFISA MTENDAJI WA KIJIJI**

Sahihi ............

Jina JUMA M. MNJINGAC

**MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI**

Zimegongwa mhuri wa Halmashauri ya Kijiji cha Muungano

Sheria Ndogo hizi zimepitishwa na kusainiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi

Tarehe 29 JULAI 2013 zianze kutumika tarehe: 1 AGOSTI 2013.

Sahihi ............

Jina GRACE MBARUKU

***MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI LINDI VIJIJINI WILAYA***

Sahihi ............

Jina MATHEI B. MAUNYA

***MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI VIJIJINI***

Zimegongwa mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi vijijini

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MUUNGANO

OFISI YA MTENDAJI KIJIJI
CHA MUUNGANO
BOX 328
LINDI
5/08/2011

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BOX 328
LINDI

YAH: KUKUTUMIA MUHTASARI WA KIKAO MAA LUMU CHA SERIKALI YA KIJIJI MUUNGANO CHA KUPITISHA MPANGO WA MATUMIZI BORA Y ARDHI KIJIJINI MUUNGANO.

Mada hiyo hapo juu yahusika na barua hii. Napenda kukutumia muhtasari wa kikao maalumu cha kupitisha mpango wa matumizi bora ya Ardhi Kijijini Muungano kilicho fanyika siku ya Tarehe 5/08/2011 Kwa barua hii nina ambatanisha na muhtasari huo.

Naomba uupokee

Ahsante

[signature]

Rashidi S. Rashidi

VEO

[stamp] ... MTENDAJI ... KIJIJI ... MUUNGANO

MAHUDHURIO YA WAJUMBE SIKU YA TAREHE 5/8/20

| NO. | JINA KAMILI | CHEO | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1. | JUMA M. NJANGALI | M/KITI | [signature] |
| 2. | RASHIDI S RASHIDI | KATIBU | [signature] |
| 3. | ISSA A. MTIMBA | MJUMBE | [signature] |
| 4. | ISSA A. MAENJELA | " | [signature] |
| 5. | ISSA R. MTAMILE | " | Mtamile |
| 6. | ISSA R. WEYA |  | R. Weya |
| 7. | RAJABU LIPILI | " | Lipili |
| 8. | RAJABU MPUJULE | " | [signature] |
| 9. | RASHIDI KITIPA | " | [signature] |
| 10. | OMARI NJEGAMA | " | [signature] |
| 11. | OMARI NAMPANYA | " | O. Nampanya |
| 12. | SALIMA KACHEMBA | " | S. Kache |
| 13. | SAIDI NAWAKO | " | [signature] |
| 14. | ABDALAH NJANGALI | " | A. njanga |
| 15. | ALY MNGAUYA | " | [signature] |
| 16. | FATU MPUJULE | " | F. mpujule |
| 17. | FATU LIKONGOLA |  | F. Likongo |
| 18. | ESHA KINDAMBA | " | E. Kinda |
| 19. | SULEIMANI MITOLE | " | [signature] |
| 20 | MOHAMEDI MATOLA | " | [signature] |
| 21 | YUSUFU MATEWELE | " | [signature] |
| 22 | BAKARI MTULE | " | B. Mtule |
| 23. | ZUBERI MTONOYA | " | Z. mtonoya |
| 24. | ZAINABU MSHAMU | " | Z. mshamu |
| 25. | KHADIJA NDEYELO | " | ndeyelo |
| 26. | BAKARI LINGOMBE | " | B. Lingombe |

MUHTASARI WA KIKAO MAALUMU ~~WA KIKAO~~ CHA WAJUMBE WA SERIKALI CHA KUPITISHA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARIDHI YA KIJIJI CHA MUUNGANO KILICHO FANYIKA SIKU YA TAREHE 5/8/2011.

AGENDA NO 1/2011 KUFUNGUA KIKAO.

Mnamo saa 6.00 Mchana mkiti alifungua kikao.

AGENDA NO 2/2011 KUPITISHA MPANGO WA MATUMIZI BORA YA ARIDHI WA KIJIJI CHA MUUNGANO.

Awali ya yote mkiti aliwafahamisha wajumbe kuwa kwenye kijiji chetu kuna mpango wa matumizi bora ya Aridhi na wajumbe kwa pamoja walikili kuwa wanafahamu kitu hicho kuwa kipo kwenye kijiji chetu. Hapo ndipo mkiti aliwaomba wajumbe - watoe ridhaa ya kupitisha mpango huo kupitia kikao hiki.

Tmeagiziwa kuwa mpango umepitishwa kwa kauli ya wajumbe wote kwani wanaamini kuwa watapata fursa nyingi kupitia mpango huu Ikiwemo na kupata hati miliki za kimila na mambo mengine mengi yanayo husu kijiji chetu.

Kamati ya matumizi bora ya Aridhi ya kijiji cha muungano ipo naye ni

1. Abdalah mohamedi Matowoke mkiti
2. Issa Abdalah Maonjela - Katibu
3. Fatu O. Mpujuk - Mjazina
4. Ashmu Mtili - mjumbe
5. Bibie Lioka - "
6. Mwanajuma Mwarauba "
7. Khadija Mngauya "
8. Omari Mtaule "
9. Tsumaili Mchaka "
10. Zuhura Masuli "
11. Shalifa Nampapali "
12. Bakari Mpiliu "

AGENDA NO 3/2011 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alisimama alitoa shukrani kwa wajumbe wote kwa kipindi walichokuwepo kwenye kikao na kutoa michango yao na kisha uamuzi saa 8.00 mchana alitoa kauli ya kukifunga.

Ahsanti

Rashidi S. Rashidi
VEO

MTENDAJI WA KIJIJI CHA MUUNGANO

Juma M. Njangari
M/kiti

MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI CHA MUUNGANO